Jumanne Agosti 11, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580307

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




UKURASA 11




## Mbaroni tuhuma kumchinja mtoto kisa wivu wa mapenzi

UKURASA 3

# Mbio za urais zashika kasi

**WAGOMBEA 12** wachukua fomu NEC, wengine zaidi leo, mmoja ajinasibu akishinda wanafunzi kula wali maharage, wazee kupewa posho... *Endelea ukurasa wa 2*




## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**ASHTAKIWA KUKUSANYA BILIONI 17/- BILA LESENI**

MFANYABIASHARA Tariq Machibya (29), maarufu kama Mr Kuku, amefikishwa mahakamani...

**UKURASA WA 4**

**TTCL YAPONGEZWA UHAKIKI PEMBEJEO**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amefurahishwa na mfumo maalum wa kuhakiki pembejeo za wakulima unaojulikana kama...

**UKURASA WA 7**

**BALOZI RUHINDA: BEN MKAPA ALIKUWA NA SIFA ZA BINADAMU**

FERDINAND Kamuntu Ruhinda, Mwandishi wa Habari, Mshauri na Mwanastratejia wa Siasa, Mhariri na Balozi wa...

## SERIKALI YAPOKEA BILIONI 17/- GAWIO CRDB

UKURASA 3

# CCM yakoleza moto panga wala rushwa

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store

**MICHEZO** YONDANI, ABDUL WAZIINGIZA VITANI GWAMBINA, NAMUNGO UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akihutubia wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT) wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza hilo, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Mbio za urais zashika kasi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBIO za kuusaka urais wa Tanzania zimeendelea kushika kasi, wagombea kutoka vyama vya siasa 12 kati ya 19 vyenye usajili wa kudumu nchini wakichukua fomu ya kwenye ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuomba uteuzi wa kuwania nafasi hiyo katika uchaguzi wa Oktoba 28 mwaka huu.

Jana, wagombea wawili walichukua fomu NEC, akiwamo wa Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Hashimu Rungwe, aliyesema kuwa endapo Watanzania watampa ridhaa, atahakikisha anatoa ruzuku kwa wakulima na posho maalum kwa ajili ya wazee nchi nzima.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa fomu akiwa na mgombea mwenza wake, Mohammed Masoud, Rungwe alisema wakulima watapatiwa ruzuku katika mazao yao kwa kuwa wanafanya kazi kubwa.

Rungwe alisema kuwa, akiwa rais, atahakikisha wazee wanapata posho maalum ili kutambua kwa vitendo mchango wao kwa taifa.

"Wazee waliitumia nchi hii, sasa wakishamaliza kuitumikia nchi hii, ndiyo tunawatupa? Hatuwezi kumtupa mzee, CHAUMMA inasema mzee atapata chakula," alisema.

Mgombea huyo ambaye uchaguzi mkuu wa mwaka huu ni wa tatu kwake kuwania nafasi hiyo, pia alisema atahakikisha wanafunzi wanakula milo yote shuleni, hasa ubwabwa na maharage.

"Nilishawaambia watoto watapata ubwabwa kwa sababu mimi niliposoma, chakula nilikuwa ninapata shule. Saa nne tu tunasikia uji ananukia, tunakunywa na saa sita tunaitishwa chakula tunakula, siku nyingine ubwabwa na nyama, siku nyingine ubwabwa na maharage kidogo. Hayo ndiyo yalikuwa maisha yetu ya shuleni wakati huo, vitu hivyo vilipotea," alisema.

Rungwe alisema anaamini wanafunzi kutofanya vizuri darasani kunatokana na kusoma wakiwa na njaa, hivyo suluhisho ni kuwapa ubwabwa shuleni.

"Mimi ninaona hawa watoto wetu tusikae tukawaambia tu 'mbona wewe umefeli?' Mimi nitaawandalia ubwabwa, hela wanazo si wanalipa kodi? Watapata fedha, zitaenda kufanya kazi hiyo. Usiniulize hela watapata wapi, watapata tu hela, wanazo hiyo ndiyo kazi yangu," alisema.

Mbali na hilo, Rungwe alisisitiza ahadi yake ya kupeleka Bahari ya Hindi makao makuu ya nchini, jijini Dodoma kwa kutumia mifereji.

"Bahari siyo mfereji mkubwa ule kutoka kule mpaka huku, watu wa huku watatengeneza namna yao ya kwenda na wa kule pia wataenda, boti zitapita hapa zitachukua watu, meli zitapita zitachukua mizigo, hicho ni kitu cha kawaida," alisema.

Alipoulizwa kuhusu wadhamini, mgombea huyo alisema ataanza kutafuta wadhamini alipozaliwa na kuzikwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Butiama mkoani Mara.

**MGOMBEA UMD**

Wakati Rungwe akimwaga ahadi zake hizo, mgombea wa UMD, Khalfan Mohamed Mazurui, naye jana alichukua fomu akiwa amefuatana na mgombea mwenza wake, Mashavu Alawi Haji, huku akisema kipaumbele cha chama hicho ni kuleta maendeleo kwa wananchi na kuwafanya kuwa na maisha laini.

Alisema kuwa kwa sasa wananchi wanaishi maisha magumu aliyoyafananisha na ugali uliolala.

"Ingawa kampeni bado hazijaanza, lakini tuna matumaini makubwa kwamba hali itakuwa nzuri na wananchi watatuelewa katika zile sera tutakazowatangazia na matumaini ya kidemokrasia na maendeleo kwa wananchi," alisema.

Mgombea huyo pia alisema serikali yake itaanzisha mfumo mpya wa kiutawala, akibainisha kuwa nchi itakuwa na majimbo badala ya mikoa iliyopo kwa sasa.

"Lengo letu ni kuifanya nchi itawalike kimajimbo na siyo kimkoa, tutaigawanya nchi kwa majimbo ili tulete maendeleo tofauti na sasa kuna mikoa mikubwa sana," alisema Mazurui.

Wiki iliyopita, NEC ilifungua rasmi pazia uchukuaji fomu hizo lililoanza Agosti 5 hadi 25 mwaka huu. Wagombea wengine waliojitokeza kuchukua fomu ni pamoja na wa Chama Cha Mapinduzi(CCM), Dk. John Magufuli, Chama cha Wakulima (AAFP), Seif Maalim Seif, Chama cha DP, Philipo Fumbo, na wa chama cha NRA, Leopord Mahona.

Wengine ni mgombea wa chama cha ACT-Wazalendo, Bernard Membe, chama cha UPDP, Twalib Kadege, mgombea wa ADC, Queen Sendiga, mgombea wa chama cha SAU, Mutamwega Mgaiwa, na mwishoni mwa wiki iliyopita, mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu alichukua fomu pamoja na Chama cha Demokrasia Makini kilichopanga kumsimamisha Cesilia Mmanga.

**CUF, CCK, NCCR**

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na NEC, leo ni zamu ya wagombea wa Chama cha Wananchi (CUF), Chama Cha Kijamii (CCK) na NCCR-Mageuzi kuchukua fomu, wakiwatangulia wagombea wa Chama cha National League for Democracy (NLD) na ADA TADEA watakaochukua fomu kesho.

DANISH REFUGEE COUNCIL

TANGAZO LA ZABUNI

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUNUNUA **VIFAA VYA KUTENGENEZEA MKAA**

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAALIKA WAZABUNI WENYE NIA **KULETA ZABUNI ZAO.**

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA **TAREHE 11.08.2020 HADI TAREHE 24.08.2020 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30** JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA +255627423991 au barua pepe jean.kabore@drc.ngo**

**ZABUNI ZITAFUNGULIWA TAREHE 27.08.2020 SAA 4:00** ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISHI.

**UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA RFQ.TZA@drc.ngo AU KULETA MOJA KWA MOJA OFISINI KIBONDO VINGINEVYO NI BATILI.**

215852002

# Samia akoleza moto panga wala rushwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amesisitiza kuwa vikao vya juu vya Chama Cha Mapinduzi (CCM) havitawaonea haya waliokiuka maadili ikiwamo rushwa katika mchakato wa kura za maoni kutafuta wagombea ubunge na udiwani.

Pia amelitaka Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania la Chama Cha Mapinduzi (UWT), kuchuja wagombea kwa haki bila kumwonea mtu aibu.

Akifungua jana bazara hilo ambalo ni maalum kwa ajili ya uchaguzi wa wabunge wa viti maalum waliopitishwa kwenye kura za maoni kwenye mikoa, Samia alisema baadhi ya maeneo kumetokea kasoro kadhaa za uchaguzi.

"Ni matumaini yangu kuwa Baraza hili Kuu litasahihisha changamoto na ukiukwaji wa taratibu uliotokea kwa kufanya mchujo wa haki bila kumuonea mtu aibu au haya, mkumbuke moja ya ahadi za chama chetu inasema 'nitasema kweli daima, fitina kwangu mwiko'," alisema.

"Mkishindwa kujipanga wenyewe vikao vya ngazi za juu ikiwamo Kamati Kuu vitalazimika kuwapanga."

Alisema vikao hivyo vitafanya hivyo ili kuhakikisha viongozi watakaokiwakilisha chama kwenye uchaguzi mkuu ni waadilifu.

"Tutafanya hivi ili kuhakikisha viongozi watakaokiwakilisha chama chetu ni waadilifu, wachapakazi na wenye kuendana na maadili ya chama na dhima yetu ya Hapa Kazi Tu inayolenga kumuinua Mtanzania mnyonge kutoka kwenye dimbwi la umaskini," alisema.

Alisema anaamini waliopita katika mchakato wa kura za maoni na kupitia ngazi mbalimbali za uchujaji ni viongozi wazuri ambao hawakukiuka taratibu na kanuni za uchaguzi ikiwamo kutoa rushwa.

"Kiongozi mzuri ni yule aliye na uwezo wa kuongoza wenzie kwa kujiamini na kushirikisha wengine na siyo mtoa rushwa au mpokea rushwa, siku zote kiongozi ni yule anayechaguliwa kwa kura nyingi na kwa ridhaa ya wananchi, na siyo kwa nguvu ya fedha," alisema.

Kadhalika, aliwataka wanawake wote wa CCM kujiandaa na kujipanga kwa uchaguzi wa dola ili kuhakikisha CCM inashinda kwa ushindi mkubwa.

Alipongeza Umoja huo kwa kuongeza idadi ya wanachama wapya kutoka 1,752,145 mwaka 2018 hadi kufikia 1,934,744 mwaka 2020.

Alikemea makundi ya uchaguzi na kutaka yavunjwe na watakaobainika kujihusisha nayo chama kitawachukulia hatua hali.

"Kipindi hiki tunapoelekea kwenye uchaguzi twende tukiwa wamoja kwa kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, Jumuiya ya wanawake ni tegemeo kubwa kwa Chama kwa kuwa wanawake tuna msimamo usioyumba na umoja wetu ni nguvu ya kutenda makuu," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa UWT Taifa, Gaudencia Kabaka, aliwataka wanawake hao kuungana kwa pamoja kuhakikisha wanakamilisha dhana ya mafiga matatu katika sanduku la kura kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Naye, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, Rodrick Mpogolo, aliwataka wanawake kuwa wamoja na kuzingatia mshikamano kama silaha ya ushindi.

## HABARI KITAIFA

# Adaiwa kumchinja mtoto wivu wa mapenzi

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

JESHI la Polisi mkoani Kagera linamshikilia Ayoub John (38), mvuvi katika kisiwa cha Chakazimbwe wilayani Muleba kwa tuhuma za kumuua kwa kumchinja mtoto wake wa kambo Aidan Greyson (3).

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alisema jana kuwa mtoto huyo wa kiume anadaiwa kuuawa na baba yake wa kambo usiku wa kuamkia Agosti 8, mwaka huu.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni ugomvi baina ya John na mke wake ambaye ni mama wa mtoto huyo, Mektirida Nestory (27). Kutokana na ugomvi huo, alisema Nestory alikimbia kwa kuhofia maisha yake na kumwacha mtoto ndani ya nyumba.

"Kulizuka ugomvi mkubwa kati ya wanandoa hawa baada ya baba mwenye nyumba kurejea nyumbani usiku akiwa amelewa. Walipigana na mama akaamua kukimbilia kwa jirani na kumwacha mtoto huyo aliyemzaa na baba mwingine kabla ya kuolewa na mtuhumiwa. Aliporejea asubuhi alikuta mtoto ameuawa," alisema.

Kamanda huyo alisema mama alikuta mtuhumiwa huyo akiwa amelala kitandani na mtoto huyo ambaye tayari alikuwa amekwishamchinja, akakimbia huku akipiga kelele kuomba msaada kwa majirani ambao walifika na kumkamata kisha kumpeleka polisi.

Alisema chanzo cha ugomvi huo uliosababisha kifo cha mtoto ni baba kumtuhumu mke wake kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na mwanamume mwingine.

Pia alisema jeshi hilo linawasaka watu watatu kwa tuhuma za kuhusika na mauaji ya Rwegoshora Leonce (55) kwa kumpiga na silaha za jadi ikiwamo fimbo baada ya kumtuhumu kuiba mkungu wa ndizi wenye thamani ya shilingi 5,000 kutoka shamba la Nassib Abdalah, mkazi wa kijiji cha Kijongo wilayani Bukoba.

Alisema watuhumiwa hao baada ya kumpiga mtu huyo, walimbeba na kumpeleka kwa mwenyekiti wa kitongoji cha Kakiri saa 5:00 usiku wa Agosti 7, mwaka huu.

Baada ya kutoka kwa mwenyekiti, alisema walimpeleka kwa mjomba wake na kumtelekeza huko na kesho yake alifariki dunia.




Waziri wa Fedha, Dk. Philip Mpango (wa nne kulia), akipokea mfano wa hundi ya gawio la Sh. bilioni 9.3 kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (watatu kushoto), kutokana na uwekezaji wa serikali ndani ya benki hiyo kupitia Mfuko wa Uwekezaji wa DANIDA kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark. Waziri Mpango pia alipokea jumla ya gawio la Sh. bilioni 17 kutoka Benki ya CRDB ikiwa ni gawio kutokana na uwekezaji wa SerikaliKkuu, taasisi na mashirika yake. Wengine ni Waziri wa TAMISEMI, Selemani Jafo (wanne kushoto), Waziri wa Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (watatu kulia), Balozi wa Denmark Nchini, Mette Dissing-Spandet (wapili kulia), Msajili wa Hazina, Athman Mbuttuka (kulia), Makamu Mwenyekiti wa Bodi Benki ya CRDB, Prof. Neema Mori (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yapokea bil. 17/- gawio CRDB

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, jana alipokea gawio la Sh. bilioni 17 linalotokana na uwekezaji wa serikali katika ya Benki ya CRDB.

Makabidhiano hayo ya hundi kifani ya gawio hilo yalifanyika katika Ofisi za Wizara ya Fedha Dodoma na kuhudhuriwa na mawaziri na viongozi mbalimbali wa taasisi na mashirika ya umma yenye hisa ndani ya benki hiyo. Dk. Mpango alipokea hundi hiyo kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya CRDB, Dk. Ally Laay.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Mpango aliipongeza benki hiyo kwa kutoa gawio kwa serikali pamoja na kupata matokeo mazuri ya fedha kwa mwaka 2019 ambayo yamewezesha kuongezeka kwa gawio kwa wanahisa, ikiwamo serikali.

"Ongezeko hili la gawio ni kiashiria tosha kwa serikali kuwa CRDB inazidi kuimarika zaidi kutokana na mikakati madhubuti ya kibiashara iliyojiwekea na jambo linalowapa moyo Watanzania na wawekezaji kuwa benki inatoa huduma bora katika jamii," alisema.

Dk. Mpango alisema fedha zilizopatikana kupitia gawio hilo zitasaidia utekelezaji wa miradi ambayo serikali imeainisha katika vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2020/2021.

"Kipekee kabisa niipongeze bodi, menejimenti na wafanyakazi wote wa CRDB kwa kazi nzuri mnayoifanya," aliongezea Dk. Mpango.

Pia aliipongeza CRDB kwa matokeo mazuri ya fedha iliyopata katika nusu ya kwanza ya mwaka huu kutokana na ongezeko la faida kwa asilimia 15 kufikia Sh. bilioni 70.4 kutoka TZS bilioni 61.1 zilizoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Akizungumzia umuhimu wa ushiriki wa taasisi za fedha katika maendeleo ya taifa, Dk. Mpango aliipongeza CRDB kwa kupunguza riba katika mikopo ili kuchochea shughulia za maendeleo nchini.

"Niwapongeze kwa kupunguza riba katika mikopo, hiki kimekuwa kilio cha muda mrefu cha serikali kwa mabenki (benki) nchini. Niyasihi (nizisihi) mabenki (benki) mengine (nyingine) kufuata nyayo hizi za benki ya CRDB," alisema Dk. Mpango.

Dk. Laay alisema gawio hilo ni sehemu ya faida ya Sh. bilioni 120.1 baada ya kodi ambayo CRDB na kampuni zake tanzu imeipata katika mwaka wa fedha 2019. Pia alisema kuwa benki hiyo itaendelea kutoa huduma bora ili kukidhi mahitaji ya wanahisa wake na wananchi kwa ujumla.

"Katika mkutano wa wanahisa uliofanyika kidijitali Juni, mwaka huu, wanahisa wa benki ya CRDB walipitisha kwa pamoja gawio la Sh. 17 kwa hisa ikiwa ni ongezeko la asilimia 112.5, hivyo kufanya gawio la mwaka huu kufikia Sh. bilioni 44.4," alisema Dk. Laay.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alimhakikishia Dk. Mpango kuwa CRDB kupitia kauli mbiu yake ya "Tupo Tayari" itaendelea kushirikiana na serikali katika kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha.

Alisema benki hiyo imejikita zaidi kwenye uwekezaji wa mifumo ya kidijitali ya kutolea huduma kama CRDB Wakala, SimBanking, SimAccount na Internet banking ambayo humsaidia mteja kupata huduma kwa urahisi, unafuu na haraka.

Akipokea gawio kutokana na uwekezaji wa halmashauri za Mbinga, Lindi, Shinyanga, Mufindi, Chunya na Rungwe, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, alizihimiza halmashauri zingine nchini kuweka katika hisa ili kupanua wigo wa mapato.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Ajira na Vijana, Jenista Mhagama, alipongeza mifuko ya jamii ya PSSSF, NSSF na ZSSF kwa uwekezaji ndani ya CRDB huku akiwataka viongozi wa mifuko hiyo kutumia gawio walilopata kuboresha utendaji kazi ili kunufaisha wanufaika wa mifuko hiyo.

# Ashtakiwa kukusanya bilioni 17/- bila leseni

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Tariq Machibya (29), maarufu kama Mr Kuku, amefikishwa mahakamani akikabiliwa na mashtaka saba likiwamo la kujihusisha na biashara ya upatu kwa kukubali na kukusanya Sh. bilioni 17 kutoka kwa umma bila leseni.

Mshtakiwa huyo ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Mr Kuku Farmer Ltd, alisomewa mashtaka yake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi Godfrey Isaya.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa Januari 2018 mpaka Mei, mwaka huu katika mahali tofauti jijini Dar es Salaam, alijihusisha na biashara ya upatu kwa kukusanya fedha kutoka kwa umma.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alikusanya fedha hizo kwa madai ya kufanya ujasiriamali wa ufugaji wa kuku na wangepata faida ya asilimia 70 ya mtaji waliowekeza kwa miezi minne ya awali na asilimia 90 ya mtaji kwa miezi sita kiasi ambacho ni kikubwa kibiashara kuliko mtaji uliowekezwa.

Wakili Wankyo alidai kati ya Januari mwaka 2018 na Mei 2020, maeneo tofauti jijini Dar es Salaam, alikubali na kupokea Sh. bilioni 17 kutoka kwa umma bila kuwa na leseni.

Ilidaiwa kwamba, kati ya Aprili 26, mwaka 2019 na Januari mwaka 2020 jijini Dar es Salaam, alijihusisha na muamala wa Sh. 6, 477,297,614.83 kwa kuzitoa kutoka kwa akaunti ya Mr Kuku iliyopo benki ya CRDB wakati akifahamu zimetokana na kosa la kujihusisha na biashara ya upatu.

Mshtakiwa huyo pia anadaiwa kwamba kati ya Januari na Machi 30, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, alitakatisha Sh. 629,249,576.36 kwa kuzitoa kutoka akaunti ya CRDB wakati akijua ziitokana na kosa la upatu. Wakili Wakyo alidai kati ya Machi 5 na Aprili 17, mwaka huu, alitakatisha Sh. 1,366,718,045.46 kwa kuzitoa kutoka akaunti ya Mr Kuku Farmers Ltd, iliyopo benki ya CRDB.

Aliongeza kuwa kati ya Januari 17 na 30, mwaka huu, jijini Dar es Salaam katika tawi la CRDB Viva Tawar, Kinondoni, Dar es Salaam, alitakatisha Dola 107,893.73 kw akuzitoa oa na kuziingiza katika akaunti ya Mr Kuku wakati akijua zilitokana na biashara ya upatu.

Wankyo alidai kati ya Machi 3 hadi 30, mwaka 2020 benki ya CRDB Water Front, Machibya alijihusisha na muamala wa dola 146, 300 na kuziingiza katika akauti ya Mr Kuku Farmers Ltd wakati akijua fedha hizo zilitokana na upatu.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, Wakili Wankyo alidai, upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kesi iliahirishwa hadi Agosti 24, mwaka huu. Mshtakiwa alipelekwa rumande kwa kuwa mashtaka ya utakatishaji hayana dhamana.

HABARI KITAIFA

# Waziri Mkuu aipongeza TTCL mfumo wa uhakiki pembejeo

**Na Mwandishi Wetu, SIMIYU**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amefurahishwa na mfumo maalum wa kuhakiki pembejeo za wakulima unaojulikana kama 'T-Hakiki' uliozinduliwa hivi karibuni na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) kuwasaidia wakulima kutambua ubora wa pembejeo kabla ya kuzitumia.

Waziri Mkuu alivutiwa na mfumo huo alipotembelea banda la TTCL kwenye maonyesho ya Nanenane Kitaifa aliyoyafunga rasmi juzi katika Viwanja vya Nyakabindi Mkoa wa Simiyu.

Alisema mfumo huo ni mzuri endapo utatumika vizuri kwa wakulima na unaweza kuwasaidia kupambana na pembejeo feki.

Akitoa maelezo kwa Waziri Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa TTCL Corporation, Waziri Kindamba, alisema mfumo huo umetokana na ubunifu wa TTCL, Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu Ukanda wa Tropiki (TPRI/TAPHPA), wakilenga kumsaidia mkulima kutambua pembejeo feki, zikiwamo dawa, mbegu na mbolea wanazotumia.

Mkurugenzi Kindamba alisema ubunifu huo umeenda sambamba na malengo ya Rais John Magufuli katika kuleta mapinduzi kwenye sekta ya kilimo.

"Uuzaji wa pembejeo bandia za kilimo una athari kubwa kiuchumi na kijamii. Kwa sasa, huduma hii itamsaidia mkulima kufahamu matumizi sahihi ya pembejeo hizo kupitia simu ya mkononi.

"T-Hakiki ni mfumo wa njia ya SMS ambapo mkulima atatakiwa kubofya *148*52# na kuingiza namba ya siri iliyopo kwenye vifungashio vya mbegu, mbolea au kwenye chupa za vifungashio vya mbegu, mbolea au kwenye chupa za viuatilifu ili kuthibitisha uhalisi wa pembejeo," alifafanua.

Katika hatua nyingine, TTCL imeibuka mshindi wa kwanza katika kipengele cha watoa huduma za mawasiliano nchini huku ikishika nafasi ya tatu katika kuwasaka washindi wa jumla wa maonyesho ya Nanenane Kitaifa mwaka huu na kukabidhiwa vikombe vya ushindi huo juzi kwenye sherehe za kuhitimisha maonyesho hayo.

TTCL ilikabidhiwa kikombe cha mshindi wa kwanza katika kipengele cha watoa huduma za mawasiliano nchini na Waziri Mkuu Majaliwa huku kile cha ushindi wa tatu wa jumla ikikabidhiwa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, kwenye hafla za ufungaji wa maonyesho hayo.



Mafundi wa CCECC, wakiendelea na upanuzi wa barabara katika makutano ya barabara ya Morogoro na Sam Nujoma, eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MARIAM MAGILI**

# Waliofariki ajali ya lori la mafuta wakumbukwa

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, jana alihudhuria ibada maalum ya kuwaombea watu waliopoteza maisha katika ajali ya moto baada ya lori la mafuta kulipuka, Agosti 10, mwaka jana.

Ibada hiyo ilihudhuriwa na viongozi wa dini, serikali na wananchi wa mkoa huo wa Morogoro.

Ajali hiyo ilisababisha vifo vya watu 115 ambao walizikwa katika makaburi ya pamoja na majeruhi 21.

Mkuu huyo wa Mkoa alisema kuwa kwa sasa serikali ya mkoa inafanyia kazi maombi ya wadau mbalimbali ya kutaka kujengwa njia ya mchepuko kwa ajili ya magari yanayobea mafuta, kemikali na sumu.

"Ni kweli kuwapo kwa njia ya mchepuko kwa ajili ya magari makubwa yanayobeba mafuta kemikali na sumu itakayopita nje ya mji, itasaidia kupunguza ajali zisizo za lazima, lakini kuna changamoto ya tabia ya watu kufuata barabara ilipo bila kujali athari zitakazo jiokeza," alisema Sanare.

Kadhalika alisema, mamlaka husika zinapaswa kuwajengea uwezo madereva wanaosafirisha mafuta umbali mrefu ili wawe na tahadahari ya ajali na kuimarishwa kwa utaratibu wa kutumia madereva wawili ili kusaidiana kipindi mmoja anapochoka.

Alisema, licha ya kuwapo kwa sheria inayowataka wamiliki wa magari makubwa yanayosafiri umbali mrefu kuwapo na madereva wawili, bado baadhi ya wamiliki wanakiuka sheria hiyo na kuwafanya madereva hao kuchoka wakiwa safarini na kusababisha ajali.

Mohamed Salum, mmoja wa majeruhi katika ajali hiyo, alisema anamshukuru Mungu kupona katika ajali hiyo pamoja na wataalamu wa afya kutoka Hospitali ya Mkoa wa Morogoro na Hospitali ya Taifa ya Mhimbili.

"Namshukuru sana Mungu kupona katika ile ajali, lakini namshukuru Rais wetu John Magufuli kwa kuboresha huduma za afya na kusaidia madaktari hasa katika hospitali ya mkoa wa Morogoro na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili wametusaidia sana na wametuhudumia vizuri," alisema Mohamed.

# Gavana BoT aitaka TADB kuinua wakulima

**Na Mwandishi Wetu, BARIADI**

GAVANA wa Benki Kuu Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, amepongeza utendaji kazi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), na kuitaka kuongeza kasi ya kuendeleza na kuwainua wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo kwa kushirikiana na benki washirika.

"TADB mpewa dhamana kubwa ya kusimamia mageuzi katika sekta ya kilimo nchini. Mnafanya kazi nzuri ya kuwawezesha wakulima wadogo kuongeza uzalishaji wa mazao," alisema Prof. Luoga.

Akizungumza kwenye maonyesho ya Nanenane ambayo kitaifa yalifanyika katika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu, Prof. Luoga alipongeza pia ushirikiano unaofanywa na TADB na benki na taasisi zingine za kibiashara kuinua sekta ya kilimo.

"Kama benki pekee ya serikali, mna kazi kubwa ya kuinua sekta ya kilimo na uchumi kwa ujumla wake kwa kuwasaidia wakulima kufanya miradi yenye tija kwa taifa na maendeleo yake," alisema Gavana Prof. Luoga.

Alionyesha pia kufurahishwa kwake na benki na taasisi mbalimbali za kifedha kwenye maonyesho hayo kwani ndiyo eneo ambalo wadau wakubwa kwenye sekta za kilimo, mifugo na uvuvi wanapatikana.

Meneja wa TADB wa Kanda ya Ziwa, Mike Granta, ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Japhet Justine, alisema benki imeshajipanga vizuri kuziinua sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi.

"Uwapo wetu hapa tumeweza kutibu kiu kubwa ya wakulima, wafugaji na wavuvi kwani wameweza kujifunza namna gani TADB inashirikiana nao katika kuziinua sekta husika na kutoa mchango katika sekta ya viwanda," alisema.

Alishukuru pia utayari wa BoT kutoa wataalamu watakaoshirikiana na TADB kuandaa na kusimamia miradi mbalimbali ya kilimo pamoja usaidizi wowote ambao utahitajika na benki katika maendeleo ya sekta ya kilimo.

Ezekiel Maduhu, mkulima wa mdogo wa pamba kutoka Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza, aliipongeza TADB kwa kufufua vyama vya ushirika kwani amevielezea kama mkombozi katika shughuli zake za kilimo.

"Nilikuja kujifunza na kujionea bidhaa na pembejeo za kilimo, lakini nimefaidika kujifunza zaidi jinsi TADB inavyofanya kazi. Ni matumaini yangu endapo wakulima wengi wataamuka kuitumia vizuri Benki ya Kilimo basi watainuka haraka," alisema.

HABARI KITAIFA

# Watoto 580,000 kupata vyeti vya kuzaliwa

**Na Mwandishi Wetu**

WATOTO 580,000 wenye umri chini ya miaka mitano, wanatarajiwa kusajiliwa na kupewa vyeti za kuzaliwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), ndani ya miezi miwili katika mikoa ya Tanga na Kilimanjaro.

Uzinduzi wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kisasa wa Usajili wa watoto chini ya miaka mitano, ulizinduliwa jana mkoani Kilimanjaro na Waziri wa Katiba na Sheria, Mwigulu Nchemba, ukiwa na lengo la kuanzisha Mfumo wa kusajili watoto wanaozaliwa kila mwezi na kusajili watoto wote walio chini ya miaka mitano katika mikoa hiyo.

Mpango huo umeanzishwa katika vituo vyote vya afya nchini zaidi ya 1,070 vya usajili ambavyo vinatoa huduma za afya ya uzazi na watoto tofauti na awali huduma hiyo ilikuwa ikipatikana ofisi za wilaya.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu na Ofisa Mkuu wa Usajili wa RITA, Emmy Hudson, alisema mfumo huo mpya utaharakisha utoaji huduma na kuifikia jamii yote nchini.

"Mfumo huu utarahisisha familia kuwezesha watoto wao kupata haki ya vyeti vya kuzaliwa baada ya kuwezeshwa na Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) , Serikali ya Canada na Kampuni ya Simu za mkononi Tigo," alisema Hudson.

Alisema kupitia mfumo huo unaotambulika kama, 'hatua moja, eneo moja' utawezesha mfumo wa kibunifu wa kukusanya takwimu.

Hudson alisema serikali imekuwa ikitekeleza mpango huo tangu mwaka 2013 kwa kushirikiana na wadau wake UNICEF, Serikali ya Canada na Tigo.

Alisema mpango huo wameanzishwa katika mikoa ya Tanga na Kilimanjaro na utaendelea katika mikoa ya Ruvuma, Morogoro, Pwani, Singida, Dodoma, Mara, Simiyu, Lindi, Mtwara, Geita, Shinyanga, Mbeya, Songwe, Mwanza, Iringa na Njombe ambako wanatarajia kuwafikia watoto wenye umri chini ya miaka mitano milioni 4.6.

Pia, alisema mfumo huo utawezesha kuongeza idadi ya Watanzania bara wanaomiliki vyeti kutoka asilimia 13 hadi asilimia 50 kwa kipindi cha miaka saba.

Kwa upande wake, Waziri Mwakilishi na Mkurugenzi kutoka Ubalozi wa Canada, Gwen Walmsley, alisema Canada inaisaidia Tanzania kwa mpango huo wa vizazi na kutoa Dola za Canada milioni 30.6 kwa utekelezaji katika mikoa 26 ya Tanzania Bara.



Wafanyakazi wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), wakifurahia kombe, baada ya kuibuka mshindi wa pili wa kundi la vyuo vikuu, wakati wa kilele cha maonyesho ya wakulima Nanenane, katika viwanja vya Nyakabindi, mkoani Simiyu, juzi. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Shule yakabidhiwa vyoo kuepuka magonjwa

**Na Mary Geofrey**

JAMII imetakiwa kulipa kipaumbele suala la usafi wa mazingira ili kuepuka madhara yatokanayo na uchafu kama magonjwa ya kuambukiza.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Afya wa Mkoa wa Dar es Salaam, Enezaeli Ayo, katika hafla ya makabidhiano ya vyoo vilivyojengwa na Kampuni ya LIXIL wanaotengeneza vyoo vya SATO kupitia kampeni ya 'Usichukulie poa, nyumba ni choo', katika Shule ya Msingi Bombambili wilayani Ilala.

Alisema serikali inafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha mazingira salama kwa jamii na wananchi wana wajibu mkubwa wa kuhakikisha suala hilo linafanikiwa.

"Pamoja na kwamba ugonjwa wa COVID-19 umepungua nchini ila tunashauriwa kupitia waraka wa afya kwa shule kwamba tunapaswa tuendelee kuweka mazingira salama kwa wanafunzi wanapokuwa shuleni," alisema Ayo.

Alieleza kuwa, choo ni sehemu ya mazingira bora ya afya inayotajwa kama sababu moja wapo inayochangia maendeleo ya ufaulu wa wanafunzi nchini.

"Serikali itaendelea kushirikiana na SATO katika kutangaza huduma wanazotoa za vyoo salama vinavyoweza kutumiwa na yoyote na vinavyopatikana kwa gharama nafuu," alisema.

Naye Mtendaji Mkuu wa SATO, Justin Mbowe, alisema lengo la taasisi hiyo ni kuendelea kusaidia taasisi na kaya zote kuwa na miundombinu salama ya vyoo.

"Mwanzoni mwa mwaka huu tulichangia vyoo 80,000 kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa ajili ya kuboresha shule na taasisi mbalimbali kwa lengo la kuendelea kuboresha vyoo vya shule ili kusaidia juhudi za serikali za kuwa na elimu bora," alisema Mbowe.

Naye Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Bombambili, Defrosa Denis, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwatafutia wadhamini ili kuendelea kumaliza changamoto zinazoikabili.

Aliishukuru SATO kwa kuwajengea vyoo salama, vinavyotumia maji kidogo, visivyotoa harufu na ambavyo jamii inayoendelea itapenda kuvitumia kwa sababu ya urahisi wake na vyenye gharama nafuu.

Aliiomba kampuni hiyo kuendelea kutoa misaada kwa sababu bado wanahitaji matundu ya vyoo 91 ili kukidhi idadi ya wanafunzi na walimu wa shule hiyo.

# TCB yasisitiza ubora kahawa

**Na Renatha Msungu, SIMIYU**

BODI ya Kahawa Tanzania (TCB), imetoa wito kwa wakulima nchini kuhakikisha kahawa yao inaongezwa thamani, ili kupata faida kutokana na zao hilo.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Kahawa wa TCB, Kajiru Kisenge, alitoa rai hiyo wakati wa maonyesho ya Siku ya Wakulima, maarufu Nanenane mkoani Simiyu.

Alisema ujumbe wao katika maonyesho hayo ni kusisitiza wakulima wawe na viwanda vidogo vya kusindika kahawa kwa ubora unaotakiwa, ili kuongeza thamani.

"Wakifanya hivi, watakuwa wanaongeza thamani ya kahawa, jambo ambalo litaongeza bei na kuwanufaisha zaidi," alisema.

Alisema wametumia maonyesho hayo kuwahamasisha wakulima namna ya kuzalisha kahawa bora yenye viwango vinavyotakiwa.

Mkurugenzi huyo alisema TCB pia ilitumia maonyesho hayo kuhamasisha kuhusu unywaji wa kahawa kwa wingi nchini, namna ya kutengeneza kinywaji hicho na faida zake mwilini.

"Watu wengi wana taswira potofu kuwa kahawa ina madhara mwilini, lakini ni kinywaji kizuri ambacho huchangamsha mwili," alisema.

Katika banda lake, bodi hiyo ilitoa fursa kwa wananchi kuonja kinywaji hicho na kuwaelekeza namna ya kukiandaa.

Mmoja wa wananchi waliotembelea banda hilo, Isaac Chenge, aliipongeza bodi hiyo kwa kutoa elimu hiyo kwa wananchi kwa kuwa wengi walidhani kahawa ina madhara mwilini.

"Mimi binafsi nilikuwa ninaogopa sana kunywa kahawa, lakini baada ya maelezo ya leo (juzi), nitaanza kutumia kahawa, ninaipenda sana harufu yake lakini nilikuwa ninaogopa kuinywa kutokana na hofu kwamba ina madhara," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wakulima, wafugaji, wavuvi dhihirisheni mliyojifunza Nanenane

KWA miaka kadhaa mfululizo wa maonyesho ya Nanenane yamekuwa yakifanyika kitaifa wilayani Bariadi mkoani Simiyu.

Kwa mara nyingine, mwaka huu maonyesho hayo yamefanyika mkoani humo katika viwanja vya Nyakabindi wilayani humo.

Maonyesho ya mwaka huu yameonyesha kuwavuta wadau wengi wa sekta za kilimo, mifugo, uvuvi pamoja na wengine kutoka nje ya sekta hizo; kwa maana ya kushiriki kikamilifu kwa njia mbalimbali zikiwamo kutoa huduma na kutembelea kwa lengo la kujifunza.

Wakati wote tangu kufunguliwa rasmi mapema mwezi huu, idadi kubwa ya wananchi na wadau kwa ujumla imejitokeza kwenye viwanja hivyo kwa ajili ya kuona bidhaa zinazozalishwa na wakulima, wafugaji na wavuvi. Mbali na kuziona bidhaa hizo, lakini jamii imejionea teknolojia mbalimbali za kisasa zinazotumika katika uzalishaji wa bidhaa bora.

Watafiti na wataalamu mbalimbali wa sekta hizo wametumia muda wao kuelezea bidhaa wanazozizalisha pamoja na kuelimisha teknolojia za kisasa zinazotumika katika uzalishaji huo kwa lengo la kuongeza kiwango cha uzalishaji wa bidhaa zenya ubora.

Kadhalika, katika kipindi chote cha maonyesho hayo ambayo yanatarajiwa kumalizika leo baada ya kuongezewa siku mbili, taasisi za umma, wakala, wizara na taasisi binafsi, zimeshiriki kwa kutoa huduma za shughuli zao sambamba na kutoa elimu kwa umma.

Vile vile, viongozi wa kitaifa walitembelea maonyesho hayo wakiwamo Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan; Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa; mawaziri, makatibu wakuu, wakuu wa mikoa, makatibu tawala kwa kutaja baadhi.

Ushauri uliotolewa na viongozi hao ulijikita katika kuwahimiza na kuwahamasisha wazalishaji wa bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi kuzalisha bidhaa zenye ubora kwa kutumia teknolojia ya kisasa kwa lengo la kukidhi viwango na kupata soko la uhakika la ndani na nje ya nchi.

Kwa upande mwingine taasisi rasmi za kifedha zikiwamo benki, zimeshauriwa kuwawezesha wazalishaji wa bidhaa hizo kwa kuwakopesha mikopo ya uhakika ili kukidhi matarajio yao.

Wajasiriamali hao nao wameshauriwa kuzitumia taasisi rasmi za kifedha kukopa kwa ajili ya kuwaepuka wakopeshaji waliotapakaa mitaani, ambao wanakopesha kwa masharti magumu, zikiwamo riba kubwa, ambazo zimewaumiza wajasiriamali wengi kwa kujikuta wanafilisika kutokana na riba kubwa zisizoeleweka.

Kama ni darasa, hakika wazalishaji wa bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi watakuwa wameelimika kwa kiasi kikubwa na vya kutosha kutokana ushauri na maelekezo yaliyotolewa na viongozi wa serikali na taasisi waliotembelea maonyesho hayo.


Suala lingine la msingi ni kwa wazalishaji kuzingatia ushauri uliokuwa ukitolewa na watafiti wa taasisi za utafiti zilizoshiriki. Kwa mfano, matumizi ya mbegu za kisasa zilizofanyiwa utafiti ambazo zina uwezo wa kutoa mazao mengi na yanayokidhi ubora.

Ushauri wetu kwa wazalishaji wa bidhaa hizo hususan wadogo na wa kati ni kuwa pamoja na kutakiwa kuzalisha kisasa, wahakikishe wanachangamkia fursa ya kwenda kukopa kwenye taasisi rasmi, ambazo mikopo yao ni ya uhakika na isiyo ya kinyonyaji.

Kwa upande wa taasisi za fedha, zihakikishe zinaweka utaratibu mzuri wa kuwakopesha wajasiriamali hao bila urasimu, kwa kuwa kuwa ni watu muhimu katika ukuaji uchumi wa taifa letu pamoja na maendeleo ya viwanda.

Tunaishauri serikali iendelee kuyaboresha maonyesho ya Nanenane ili yashirikishe idadi kubwa ya wakulima, wafugaji na wavuvi na kuwapatia ujuzi, uzoefu na teknolojia ya kuzalisha bidhaa kwa njia ya kisasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# TEHAMA sasa ni wajibu, haikwepeki

TEKNOLOJIA ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kwa sasa ni moja ya kigezo kinachotumika kutathmini ubora wa shule za sekondari, lengo likiwa ni kuhamasisha utumiaji wa teknolojia hiyo shuleni.

Kwa maana hiyo, suala la kutumia TEHAMA ni muhimu, hasa kwa shule ambazo walimu wake wamepata mafunzo ya jinsi ya kutumia teknolojia hiyo kwa manufaa ya wanafunzi.

TEHAMA pia haiishii kwenye shule tu bali inatajwa kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji na uendelezaji wa shughuli mbalimbali, na hutumika katika maeneo mengi yakiwamo ya kibiashara.

Hivyo kutokana na ukuaji wa teknolojia na kuongezeka kwa matumizi ya simu za mkononi na mitandao ya kijamii, imekuwa ni rahisi watu kuwasiliana na hata kufanikisha shughuli zao za kila siku.

Kwa mfano, kutokana na ukuaji wa teknolojia wafanyabiashara wengi wanatafuta masoko kupitia teknolojia ya mawasiliano kama vile mitandao ya kijamii ikiwamo whatsup, facebook na instagram.

Mfanyabiashara anapotumia njia hiyo, anaweza kuuza bidhaa au huduma mtandaoni kwa kuweka bidhaa zake pamoja na taarifa zote muhimu kama bei, mawasiliano na namna gani mteja anaweza kuipata.

Hivyo, kutokana na umuhimu huo wa TEHAMA, wanawake wanaofanya biashara nje ya mikapa ya Tanzania, wanahimizwa kuitumia ili wawafikie wateja wengi kirahisi na tena kwa muda mfupi.

Huo ni ushauri wa Mhadhiri wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Mariam Tambwe, kwa wanawake hao wakati akitoa mafunzo ya siku tano ya kuwajengea uwezo yaliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

TEHAMA pia inatajwa kutumika katika utunzaji wa kumbukumbu, ambao kwa ujumla wake ni kwamba unamsaidia mtu kuona mwenendo wa biashara yake na kulipia malipo mbalimbali ikiwamo kodi ya mapato ya serikali.

Ukuaji wa teknolojia umerahisisha utunzaji wa kumbukumbu za biashara, kwa kuwa unaweza kufanyika kupitia mfumo maalumu wa kidigitali, ambao unamsaidia mtu kutunza kumbukumbu za biashara yake kwa haraka na kiurahisi.

Kwa mujibu wa mhadhiri huyo, kupitia teknolojia hiyo mtu anaweza kupata elimu ya biashara kwa kujifunza mambo mengi yahusuyo biashara ingawa kuna changamoto kadhaa ikiwa ujuzi mdogo wa matumizi ya teknolojia hiyo.

Aidha, suala la matumizi mabaya ya teknolojia nalo linatajwa kuchangia upotevu wa muda, kutoelewa lugha ya Kiingereza nalo ni tatizo lingine kwa baadhi ya watu hali ambayo inasababisha wakwepe kuitumia.

Bila kuzingatia ubunifu kwa kutumia TEHAMA, wanaweza kukwama katika biashara zao, kwa vile anasema, baadhi ya wanawake hutumia mitandao kujianika kwa mambo yasiyofaa badala ya kutangaza shughuli zao.

Wote hao wanapaswa kutambua kuwa teknolojia hiyo ni mkombozi kwa wale wanaoitumia inavyotakiwa, hivyo wafanyabiashara wanaotaka kupata mafanikio ni muhimu wachukue hatua za kuitumia kwa usahihi.

Msisitizo zaidi ni kwamba, katika karne hii, TEHAMA haikwepeki, hivyo kinachotakiwa ni kila mwanamke kwenda na wakati kama anavyobainisha Ofisa Programu Msaidizi Idara ya Habari TGNP, Jackson Malangalila.

Anaweka wazi kuwa mitandao ya kijamii inatumiwa na wafanyabiashara kubadilishana mawazo, uzoefu na mambo mengine ya muhimu, kwa ajili ya maendeleo ya shughuli zao za kila siku.

Anakariri taarifa za Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) kwamba, asilimia 25 ya Watanzania, wanatumia mitandao ya kijamii kama jukwaa la kuwaunganisha katika shughuli zao mbalimbali.

Hivyo wanawake waliopata mafunzo hawana budi kwenda na wakati, huku TGNP ikiweka milango wazi kwa ajili ya kuwafundisha jinsi ya kufungua barua pepe na namna ya kutumia mitandao ya kijamii.

Kwa kutumia teknolojia hiyo wanawake hao watanufaika na mambo mbalimbali ikiwamo kuboresha huduma kwa wateja, kudhibiti gharama na kuleta mabadiliko katika biashara na soko kwa ujumla.

MAKALA

# Balozi Ruhinda: Ben Mkapa alikuwa na sifa zote nzuri za binadamu

- Alikuwa mnyenyekevu, hakupenda makuu wala sifa
- Aliheshimu na kukubali fikra tofauti za wengine
- Hata mimi hatukukubaliana kila kitu, lakini tulibakia marafiki



Balozi Ferdinand Ruhinda



Hayati Benjamin Mkapa, Rais wa Tatu wa Tanzania

**Na Waandishi Maalum**

FERDINAND Kamuntu Ruhinda, Mwandishi wa Habari, Mshauri na Mwanastratejia wa Siasa, Mhariri na Balozi wa Tanzania katika nchi za Canada na China, alikuwa rafiki wa karibu wa Hayati Benjamin Mkapa, Rais wa Tatu wa Tanzania, aliyefariki dunia Julai 23, mwaka huu na kuzikwa Julai 29 kijijini kwao Lupaso, Mtwara. Baada ya mazishi, Mzee Ruhinda, aliamua kutoa ushuhuda, hadharani, kuhusu rafiki yake wa zaidi ya miaka 50. Hii ni sehemu ya kwanza ya ushuhuda huo unaotolewa katika sehemu tatu.

"Nimewaombeni mje kunisikiliza. Mnisaidie. Nataka kutoa ushuhuda, hadharani, kuhusu Benjamin Mkapa, rafiki yangu, ndugu yangu." Hayo ndiyo yalikuwa maneno ya ufunguzi ya Balozi Mzee Ferdinand Ruhinda katika mazungumzo yake wiki iliyopita na waandishi wa habari watatu waandamizi.

"Kifo chake kimenisikitisha na kunihuzunisha sana. Sina maneno sahihi na mwafaka kuelezea huzuni na masikitisho yangu. I will miss him. I will miss him very much. Tulikuwa familia. Nilipopata matatizo ya kuugua, alinisaidia sana. Binafsi, kwa kweli amenisaidia mno, na mambo mengine siwezi hata kuyasema hadharani. Sitaki kujenga tahayari watu wengine. Sikuweza kushiriki kimwili katika msiba, lakini baada tu ya msiba kutokea nimezungumza na mke wake," anasema Balozi Ruhinda na kuongeza:

"Siku moja kabla ya kifo chake, Ben alikuja kuniona, kama ambavyo ilikuwa kawaida yake ya kuja kuniona. Alikuwa na utaratibu wa kuja kunijulia hali kila wiki hapa nyumbani. Alikaa hapo mlipokaa nyie. Hakukaa sana. Alikuja kunieleza yaliyokuwa yamejiri katika Mkutano Mkuu wa CCM kule Dodoma. Akaniambia pia wakati yuko Dodoma alikuwa ameshiriki mazishi ya Mzee wetu, Job Lusinde. Kama nilivyosema, zamu hii hakukaa muda mrefu, kama ilivyokuwa kawaida yake."

Anasimulia zaidi Mzee Ruhinda: "Kwa kweli, ni kama vile alikuja kuniaga. Sikujua kama sitamwona wala kuzungumza naye tena. Aliniambia hajisikii vizuri, anaumwa. Nami nilimwona hali yake, nikamshauri tusikae sana kwenye mazungumzo, bali aende hospitali kujipima afya yake," alisimulia Mzee Ruhinda na kukaa kimya kwa dakika tatu hivi, akijaribu kudhibiti na kutuliza hisia zake.

Tangu kutokea msiba, Ijumaa ya Julai 23, mwaka huu, 2020, masikitiko na huzuni ya kifo cha Ben, ndivyo vilimfanya Mzee Ruhinda kwanza akae kimya, aomboleze kifo cha rafiki na ndugu yake, na kusubiri mazishi yafanyike kabla ya kutoa ushuhuda wake. "Sikutaka kushiriki kwenye kneejerk reactions (kauli za hapo kwa hapo na kukurupuka)."

Hakuna shaka kuwa Rais wa Tatu wa Tanzania, Mzee Benjamin William Mkapa, katika maisha yake marefu, na utumishi wake wa kutukuta, na wenye shughuli nyingi za umma, alikuwa na marafiki wengi. Wengine wa miaka mingi, tokea shule, kama vile akina Mzee John Kambona na Mzee Philip Magani, ambao alisoma nao Ndanda na wote bado wanaishi.

Hata hivyo, pengine, hakuna mtu alikuwa rafiki wa karibu zaidi (Wahaya wanasema fanfe - yaani marafiki wa kufa pamoja), na aliyeamini naye, kuliko Ferdinand Kamuntu Ruhinda, mtumishi mwingine wa kutukuka na wa miaka mingi wa umma.

"Nilikutana na Benjamin Mkapa kwa mara ya kwanza, mwaka 1966, miaka 54 iliyopita, tukiwa bado vijana. Tokea wakati huo, tumekuwa marafiki. Tuliaminiana sana. Nadhani sitakosea kusema kuwa tokea nijuane naye, haikupata kupita wiki mbili bila kukutana naye, ana kwa ana, ama kuzungumza naye kwa simu, ama kwa mawasiliano ya aina nyingine. Na msinielewe vibaya, Ben alikuwa na marafiki wengi, na wa karibu, siyo mimi peke yangu," anasema Balozi Ruhinda.

Anaongeza: "Tulikutana katika mazingira ya kazi na tukawa marafiki wa kikazi na nje ya kazi. Wakati huo mimi nimeajiriwa kama mwandishi wa habari katika chumba cha habari cha Tanganyika Broadcasting Corporation (TBC), wakati huo."

"Yeye, Ben alikuwa anakuja kusoma habari za Kiingereza, wakati wa muda wake nje ya kazi. Mimi nilikuwa mmoja wa watu waliokuwa wanatayarisha habari. Aliipenda kazi yangu na urafiki wetu ulianzia hapo. Nimemfahamu kwa muda mrefu sana, zaidi ya miaka 50. Kwa kweli, uhusiano wetu ulikuwa zaidi ya urafiki. Tulikuwa ndugu."

Mzee Ruhinda anakiri kuwa ni vigumu kueleza, kwa ufasaha, nini hasa lililowavuta yeye na Mzee Mkapa kuwa marafiki kiasi hicho.

"Tulikuwa watu tofauti sana mwanzoni. Sote tukitokea pande mbili tofauti kabisa za nchi... pembezoni mwa nchi. Mmoja akitokea Kaskazini Magharibi kabisa na mwingine Kusini kabisa mwa nchi yetu. Mmoja anatokea Mto Ruvuma na mwingine akitokea Mto Kagera. Tuliunganishwa hasa na haiba zetu za kimaisha na kisiasa."

Anafafanua zaidi: "Mwaka mmoja tu, baada ya kuwa nimejuana naye, nilijiunga na Gazeti la Nationalist lililokuwa linachapishwa pamoja na Gazeti la Kiswahili la Uhuru, ambako yeye alikuwa Mhariri Mtendaji. Nikafanya kazi chini yake, kwanza nikiwa Msanifu Habari (Sub-Editor), na baadaye kama Mhariri wa Habari (News Editor)."

"Utaona kuwa urafiki wetu ulianzia kwenye shughuli za uandishi wa habari. Urafiki wetu pia ulikuwa wa kisiasa. Kama mnavyojua nyie, uandishi wa habari hauna tofauti kubwa na siasa. Baadaye, mwenzangu akaingia moja kwa moja kwenye siasa. Mimi nikabakia kwenye uandishi wa habari, lakini urafiki wetu ukabakia pale pale na kuzidi kukomaa," anasema Mzee Ruhinda.

Kwa sababu ya haiba na tabia yake kuu ya kukataa kusifiwa, wala kujitukuza, Mzee Ruhinda anakomea hapo kusimulia maisha yake binafsi. Lakini, alikuwa ni yeye alimyemrithi Benjamin Mkapa katika nafasi ya Mhariri Mtendaji wa Magazeti ya Chama (TANU) mwaka 1972, wakati Mzee Mkapa alipoteuliwa kuwa Mhariri Mtendaji wa Magazeti ya Serikali, baada ya kutaifishwa kwa Gazeti la The Standard kutoka kampuni ya kigeni ya LONRHO (London-Rhodesia), iliyokuwa inamilikiwa na mfanyabiashara maarufu wa Kiingereza, Tiny Rowlands.

Baadaye, mwaka 1976, Ferdinand Ruhinda alimrithi tena Benjamin Mkapa kwenye nafasi ya Uhariri Mtendaji wa Magazeti ya Serikali ya Daily News na magazeti dada. Kuanzia kwenye miaka ya mwanzo ya 1980 mpaka alipostaafu utumishi wa umma, Mzee Ruhinda akafanya kazi chini na kwa karibu na Mzee Mkapa katika nafasi za Naibu Balozi wa Tanzania Sweden, na Balozi Canada na katika Jamhuri ya Watu wa China.

Uteuzi wa Mzee Ruhinda kutumikia katika nafasi ya juu kabisa ya uwakilishi wa Tanzania kwenye nchi ambazo zilikuwa na uhusiano mzuri, wa karibu sana, na wa miaka mingi na Tanzania, unathibitisha jinsi Mzee Mkapa pia alivyomwamini Balozi Ruhinda. Kwa maana ya kwamba, hata kama Mzee Mkapa yeye hakumteua moja kwa moja Mzee Ruhinda kushika nafasi hizo, bado uteuzi huo usingefanywa na marais JK Nyerere na Ali Hassan Mwinyi, bila ushauri na ushawishi wa Mzee Mkapa, akiwa Waziri wa Mambo ya Nje.

Balozi Ruhinda anasema kuwa hawezi kumsemea Hayati Mkapa kwenye kila eneo kwa sababu, kwa bahati nzuri, Rais huyo mstaafu amejisemea mwenyewe vizuri katika kitabu chake cha My Life, My Purpose, kilichozinduliwa miezi minane kabla ya mauti yake. Lakini Mzee Ruhinda anamwelezea Mzee Mkapa ifuatavyo:

"Nataka kusema kile ambacho hakukisema katika kitabu chake kwa sababu ya tabia yake ya kukataa kujikweza. Ben alikuwa mtu na binadamu kamilifu, kwa kadri inavyowezekana kwa binadamu. Kila sifa nzuri ya binadamu, Benjamin Mkapa alikuwa nayo," anaeleza Mzee Ruhinda na kuongeza:

"Wapo wataosema kuwa namsifia Ben kwa sababu alikuwa rafiki yangu. Kweli, Ben alikuwa rafiki yangu. Lakini urafiki wetu haufuti ama kuondoa sifa zake nyingi. Ben aliheshimu sana fikra tofauti na zake, hata kama hakukubaliana nazo. Hii ni sifa ambayo haijitokezi vizuri katika kitabu chake."

"Ben alikuwa humble, mnyenyekevu, asiyependa makuu. Wapo wanaosema kuwa alikuwa na jeuri na kiburi cha usomi (intellectual arrogance). Kwangu mimi, madai hayo ni tofauti tu ya mawazo na maoni binafsi ya watu (difference of opinion)."

Anaongeza Mzee Ruhinda: "Sifa ya kuheshimu tofauti ya mawazo ni sifa muhimu sana kwa kiongozi. Sifa hii, inafaa kwa viongozi wetu wa sasa na wajao. Ni muhimu waikubali sifa hiyo na kuiiga. Dunia hii, watu tuko wengi, na ili tuishi pamoja na kwa amani, ni lazima tuheshimiane, hata kama hatukubaliani. Huu ni wajibu mkubwa zaidi kwa viongozi kwa sababu wao ndio kioo cha jamii."

Mzee Ruhinda anasimulia kuwa wala tabia ya Benjamin Mkapa kuheshimu mawazo tofauti haikuanza aliposhika nafasi za juu za uongozi. Anasema kuwa tabia hiyo, alikuwa nayo maisha yake yote:

"Sijui kama jambo hilo naweza kulisema vizuri, ili nieleweke ipasavyo: Akiwa Mhariri wa Magazeti ya Chama na Serikali, akiwa Waziri, akiwa Balozi na akiwa Rais, Benjamin Mkapa alihimili na kuvumilia mawazo na maoni tofauti. Hata kwenye uvumilivu wake, yapo mawazo na maoni aliyakubali, na yapo mengine aliyakataa. Kubwa ni kwamba hata aliyoyakataa hayakuwa chanzo cha chuki kwa waliyoyatoa. Ndiyo maana wakati wa utawala wake, viongozi wa vyama vya upinzani walipata fursa ya kufanya kazi zao vizuri na hata magazeti yalipanuka sana."

"Kwake yeye, mawazo tofauti hayakuwa chanzo cha uadui wala chuki. Hiyo ndiyo ilikuwa tabia na hulka yake ya maisha. Hiyo ndiyo principle, yaani msingi mkuu wa mahusiano yake na binadamu wenzake. Na hilo ndilo urithi mkuu anayowaachia wanasiasa na viongozi wa sasa na wajao wa nchi yetu."

Mzee Ruhinda anasema kuwa hata wao kama marafiki hawakukubaliana kuhusu kila kitu pamoja na kuwa na tabia ya kujadili mambo mbalimbali kila walipokutana. Anafafanua:

"Muda mwingi tulijadili mambo mbalimbali. Mengine tulikubaliana na mengine tulitofautiana. Jambo moja, kwa mfano, ambalo tulitofautiana wakati wote ilikuwa kuhusu madaraka ya Rais, na hasa uteuzi wa watu kushika nafasi mbalimbali. Mimi niliamini na naamini kuwa Rais anateua watu wengi mno na hakuna utaratibu mzuri wa kumsaidia kuwachuja. Anateua Baraza la Mawaziri, anateua ma-RC, anateua ma-DC. Wote karibu kutoka chama chake."

Anaendelea: "Iko siku moja, alimteua mtu mmoja kuwa Mbunge. Simtaji jina. Mimi nikamwendea na kumwuliza 'je, unamjua vizuri mtu huyo?' Naye akasema kuwa alikuwa hamjui vizuri. Mimi nikamweleza nilivyokuwa namjua yule mtu. Ben alisikitika sana. Lakini maji yalikuwa tayari yamemwagika."

"Siyo lazima tuwe na Katiba mpya kubadilisha jambo hili. Lakini ni jambo lina uwezekano wa hatari kubwa. Tumeona katika nchi za jirani, marais wakiteua wake zao kuwa mawaziri," anasisitiza Mzee Ruhinda.

- ***Makala hii imeandaliwa na waandishi waandamizi nchini. Salva Rweyemamu na Saidi Nguba kwa sasa wanaongoza Kampuni ya Mawasiliano ya Pioneer Communications na Tido Mhando ni Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Habari ya Azam Media. Usikose sehemu ya pili ya makala hii: Uongozi wa Mkapa na Uchaguzi Mkuu wa 1995 na nafasi za Jakaya Kikwete, Salim Ahmed Salim na Augustine Mrema katika uchaguzi huo.***

# HABARI KITAIFA

## Gereji bubu marufuku makazi ya watu

Na Shaban Njia, KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, imeagiza kufungwa kwa gereji bubu katikati ya makazi ya watu ili kuepuka majanga ya moto wakati wa shughuli za uchomeleaji.

Pia imemwagiza Ofisa Mipango Miji wa Halmashauri ya Mji wa Kahama kutekeleza uhamishaji wa gereji hizo kwa muda wa wiki mbili na kuelekea katika maeneo ya viwanja yaliyotengwa na halmashauri.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alitoa kauli hiyo baada ya kutokea kwa tukio la kulipuka kwa tangi la mafuta la gari lenye namba za usajili T.293 BEZ lililokuwa likifanyiwa matengenezo katika moja ya gereji bubu iliyopo mtaa wa Bijampola, wilayani hapo.

Macha alisema, serikali imeamua kuzifunga gereji bubu zote zilizopo ndani ya makazi ya watu maeneo ya Binjampola na kujiridhisha kama zimesajiliwa kisheria ili kudhibiti ajali zitokanazo na milipuko ya moto wakati wakiendelea na shughuli za uchomeleaji magari na matangi.

"Kila mahali penye gereji ni lazima pahakikiwe kama wahusika wanavibali vya kufanya shughuli hizo, tuzifunge gereji zote ambazo hazipo kisheria na serikali haiwezi kukubali kila eneo mjini hapa liwe la kutengenezea magari tu," alisema Macha.

"Idara ya Mipango Miji inapaswa kuhakikisha inatenga maeneo rasmi kwa ajili ya gereji kama ilivyokuwa kwenye viwanda vya mbao, ili kudhibiti utengenezaji holela wa magari ya mafuta katika makazi ya watu ambayo yanaweza kusababisha madhara yanapolipuka wakati yakifanyiwa marekebisho," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Kahama, Hanafi Mkilindi, alisema, kuanzia Agosti 12, watafanya ukaguzi katika gereji zote zilizopo katikati ya makazi ili kujiridhisha kama wana vifaa vya kukabiliana na majanga ya moto.

Bilali Musa, mkazi wa kata ya Nyihogo, alishauri Halmashauri ya Mji wa Kahama, kutenga maeneo kwa ajili ya gereji ya malori ya mafuta nje ya Mji kama walivyotenga eneo la viwanda Dodoma na kuzuia uegeshaji holela wa magari ya mizigo pembeni ya barabara.

## Wauzaji chakula, vipodozi watakiwa kusajili majengo

Na Mwandishi Wetu, BARIADI

SHIRIKA la Viwanda Tanzania (TBS), limewataka wafanyabiashara wanaofanya biashara ya chakula na vipodozi kufanya usajili wa majengo ya biashara ili watimize takwa la kisheria linalowataka kufanya hivyo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkaguzi wa TBS Kanda ya Ziwa, Nelson Mugema, katika Maonyesho ya 27 ya Wakulima (Nanenane), yaliyomalizika juzi mjini hapa.

Mugema alisema usajili wa majengo ya biashara na bidhaa ni takwa la kisheria ambalo lazima litekelezwe kwa mtu yeyote ambaye anajihusisha na biashara ya bidhaa za chakula na vipodozi kama inavyoelezwa katika Sheria ya Viwango Na. 2 ya Mwaka 2009.

"Sheria hii pia inakataza kuzalisha bidhaa za chakula au vipodozi kwa ajili ya kuuza, kusambaza au kuhifadhi katika majengo ambayo hayajasajiliwa, sheria hii inakataza mtu yeyote kuzalisha, kuagiza kutoka nje, kusambaza, kuuza au kutangaza bidhaa za vyakula na vipodozi ambazo hazijasajiliwa na TBS," alisema.

Alisema mtu yeyote anayehitaji kuuza, kuhifadhi bidhaa za chakula na vipodozi lazima majengo yake yasajiliwe na TBS kabla ya kuanza kufanya biashara hiyo.

Mugema pia alisema kila mfanyabiashara anatakiwa kukata leseni ya biashara kwa ajili ya bidhaa hizi maalum ambayo hukatwa kila baada ya mwaka mmoja.

"Kwa TBS wafanyabiashara kuzingatia takwa hili la kisheria kwa hiari ni njia muhimu sana ya kuwalinda walaji kutumia bidhaa ambazo sio salama kwa afya zao," aliongeza.

Pia aliwakumbusha wazalishaji na wadau wengine kuhusu kuhamishwa kwa shughuli zote zinazohusisha uthibitisho wa ubora na usalama wa bidhaa za chakula na vipodozi zilizokuwa zinafanywa na iliyokuwa Mamlaka ya Dawa na Chakula (TFDA) kwenda TBS kuanzia mwezi wa saba mwaka jana.

Mkaguzi huyo wa TBS aliongeza kusema kuwa huduma za usajili wa bidhaa na majengo zimekuwa zikitolewa katika maonyesho ya Nanenane, lakini kwa wale ambao watashindwa kufanya hivyo basi wanaweza kwenda katika ofisi za kanda za TBS zilizopo eneo walipo au kujisajili kwa njia ya mtandao kwenye tovuti ya TBS.

Alisema ushiriki wao katika maonyesho ya mwaka huu imekuwa fursa muhimu sana katika kutoa elimu kwa wakulima na wafugaji juu ya uthibitisho wa ubora wa bidhaa zao ili kuongeza thamani ikiwa ni kigezo muhimu sana katika kuuza kwenye soko la Afrika Mashariki na masoko mengine.

"Pia tulitumia fursa hii ya maonyesho ya wakulima kutoa elimu ya namna ya kuhifadhi bidhaa za chakula ili kuzuia kusambaa kwa sumu kuvu katika chakula, viungo, mbegu za mafuta na kakao kabla na baada ya kuvuna," alisema.


MAGAMBAZI GOLD MINING LIMITED

EMPLOYMENT OPPORTUNITY FOR MECHANICAL ENGINEER

**QUALIFICATION:**
1. Degree in mechanical engineering
2. Minimum 5 years' experience in operation and maintenance of heavy equipment & motor vehicles.

**JOB DESCRIPTION:**
1. To formulate long term plans and objectives to manage the efficiency of the Workshop and reduce downtime.
2. To make recommendations to the Management regarding the acquisition and disposal of equipment and vehicles.
3. To co-ordinate equipment workshop functions for repairs and preventive maintenance and servicing according to manufacturer's specifications and recommendations.
4. To advice on technical matters related to equipment and machinery.
5. To coordinate with the technical office to finalize purchases for new equipment/vehicles and respective spares.
6. To develop, review and approve procedures and practices for the efficient operation of the workshop within the Company's guidelines and framework.

**APPLICATION PROCEDURES:**
Applicant should attached the following documents:-
1. Application letter
2. Curriculum Vitae (CV)
3. Introduction letter from applicant's residence (local government)
4. Letters from two guarantor's of the applicant.
5. Introduction letter from guarantor's residence (local government)
6. Two photos (Passport size)
7. Photocopies of relevant certificates i.e. Education etc.

Application should be submitted through post address, email, or delivered direct at the office below not less than 20th August 2020

THE HUMAN RESOURCE OFFICER, PMM ESTATES (2001) LTD, NYERERE ROAD, NEXT TO CFAO MOTORS, P.O, BOX 33790 DAR ES SALAAM EMAIL; hrm@pmmicd.com.

115851002



MAGAMBAZI GOLD MINING LIMITED

SECURITY MANAGER (1POST)

**QUALIFICATION:**
1. All applicants must be Citizens of Tanzania generally with an age not above 45years of age
2. Proven experience at least 5 years as security manager or similar position.
3. Applicant should not have criminal records.
4. Applicant should be a graduate.
5. Committed and reliable.

**DUTIES AND RESPONSIBILITIES:**
1. Develop and implement security policies, protocols and procedures
2. Control budgets for security operations and monitor expenses
3. Investigate and resolve issues
4. Create reports for management on security status
5. Attend meetings with other managers to determine operational needs

**APPLICATION PROCEDURES:**
1. Applicants should attach the following documents:-
2. Application letter
3. Applicants must attach an up-to-date Curriculum Vitae (CV) having reliable contacts; postal address/post code, e-mail and telephone numbers;
4. Introduction letter from applicant's residence (local government)
5. Letters from two guarantor's of the applicant.
6. Introduction letter from guarantor's residence (local government)
7. Two photos (Passport size)
8. Photocopies of relevant certificates i.e. Education etc.

Application should be submitted through postal address, email, or delivered direct at the office below;

THE HUMAN RESOURCE OFFICER, PMM ESTATES (2001) LTD, NYERERE ROAD, NEXT TO CFAO MOTORS, P.O, BOX 33790 DAR ES SALAAM EMAIL; hrm@pmmicd.com.

Deadline for application is 20th August, 2020

115851002



MAGAMBAZI GOLD MINING LIMITED

CAMP MANAGER (1POST)

**QUALIFICATION:**
1. All applicants must be Citizens of Tanzania generally with an age not above 45years of age
2. Experience of 5 years in management and supervision of others; ability to take a strong leadership roles.
3. Basic computer skills including spreadsheets, word processing, and email.
4. Applicant should not have criminal records.
5. Diploma and above preferably

**DUTIES AND RESPONSIBILITIES:**
1. Responsible for the implementation of the camp activities as designated by the Top Manager
2. Ability to address problems quickly and effectively
3. Attend meetings with other managers to determine operational needs
4. Purchase any additional camp supplies, as directed by manager, that are needed beyond the regular ordering of food and camp supplies.
5. Manage all permanent camp facilities, check conditions of campgrounds before and after each group; inform personnel of needed repairs and equipment
6. Supervise all camp staff and assign additional duties as needed.

**APPLICATION PROCEDURES:**
1. Applicants should attach the following documents:-
2. Application letter
3. Applicants must attach an up-to-date Curriculum Vitae (CV) having reliable contacts; postal address/post code, e-mail and telephone numbers;
4. Introduction letter from applicant's residence (local government)
5. Letters from two guarantor's of the applicant.
6. Introduction letter from guarantor's residence (local government)
7. Two photos (Passport size)
8. Photocopies of relevant certificates i.e. Education etc. Application should be submitted through postal address, email, or delivered direct at the office below;

THE HUMAN RESOURCE OFFICER, PMM ESTATES (2001) LTD, NYERERE ROAD, NEXT TO CFAO MOTORS, P.O, BOX 33790 DAR ES SALAAM EMAIL; hrm@pmmicd.com.

Deadline for application is 20th August, 2020

115851002

# Kasi ya ukarabati barabara yaridhisha

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mfuko wa Barabara imesema imeridhishwa na utekelezaji wa ukarabati unaofanywa na Wakala wa Barabara (TANROADS) katika barabara ya Malendegu- Nangurukuru hadi Mbwemkulu iliyokuwa imeharibika kabla ya msimu wa korosho na mvua nyingine kuanza.

Aidha, imeutaka wakala huo kuhakikisha wanazingatia ukarabati wa barabara zote nchini kwa kuzingatia mabadiliko ya tabia nchi.

Hayo aliyaeleza Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Joseph Haule, wakati wajumbe wa bodi walipopita kukagua barabara ya Dar es Salaam-Lindi-Mtwara ili kuona uharibifu uliojitokeza sambamba na kukagua maendeleo ya ukarabati wa maeneo yaliyoharibiwa na mvua.

"Hakikisheni mnakarabati barabara hii kwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi kwani mvua zilizonyesha mwaka jana zinaweza kijirudia kipindi kingine, hivyo kuleta athari kubwa... mzingatie uwekaji wa mitaro katika maeneo korofi yote," alisema Haule.

Aliongeza kuwa bodi inasubiria mapitio ya mapendekezo mapya katika kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2020/21 kutokana na changamoto zilizojitokeza katika mkoa huo na kubadilisha vipaumbele ili kuweka msisitizo au mkazo katika maeneo yenye matatizo makubwa.

"Kwa sababu mwaka wa fedha umeshaanza ni vizuri TANROADS kuangalia tena kama kuna mapendekezo ya bajeti juu ya suala hili kwa makini katika ukarabati wa ushoroba wa barabara hii ambayo iliathirika sana na sisi tutayapokea na kuyafanyia maamuzi haraka," alisisitiza Haule.

Vilevile, bodi hiyo imeridhishwa na hatua iliyofikiwa ya ukarabati huo na kumhakikishia wakala huo kuwapa ushirikiano wa hali ya juu ili kuhakikisha kipande kinachohitajika cha matengenezo chenye urefu wa kilometa 2.5 kinakamilika na baadaye kukamilisha kilometa 30 zilizobakia katika sehemu hiyo.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa ukarabati wa barabara hiyo, Kaimu Meneja wa TANROADS mkoa wa Lindi, Mhandisi Ephata Mlavi, alieleza kuwa mpaka sasa wameshapata mkandarasi na wameshaanza kazi katika maeneo korofi yenye mashimo makubwa na katika maeneo ambayo lami ilikuwa imetoka ndani ya wiki mbili watakuwa wameshairudisha.

Naye Mkurugenzi wa Barabara kutoka Sekta ya Ujenzi ambaye ni mjumbe wa bodi hiyo, Mhandisi Rogatius Mativila, alisema serikali ilitumia Sh. bilioni 40 katika kukarabati maeneo yaliyoharibiwa na mvua katika mwaka wa fedha 2019/20, hivyo wizara itahakikisha inaweka sawa bajeti ya matengenezo ili kuhakikisha barabara zinakarabatiwa kwa wakati ili kuondoa usumbufu wa usafirishaji wa abiria na mizigo.

# JKT yafichua siri kuibuka kinara kitaifa Nanenane

**Na Ashton Balaigwa,** BARIADI

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limeshinda ushindi wa kwanza wa jumla kitaifa katika Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) mwaka 2020 yaliyofanyika katika viwanja vya Nyakabindi katika mkoa wa Simiyu.

Aidha, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeshinda nafasi ya kwanza kitaifa katika kipengele cha kushindanisha taasisi za utafiti nchini na kukabidhiwa zawadi.

**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeshinda nafasi ya kwanza kitaifa katika kipengele cha kushindanisha taasisi za utafiti nchini.**

Akizungumza baada ya kukabidhiwa kombe la ushindi wa jumla na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati wa kilele cha maonyesho hayo, Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Charles Mbuge, alisema ushindi huo umetokana na utekelezaji wa maagizo yanatolewa na maofisa wake.

Alisema JKT kwa kutumia taasisi zake inazoziongoza katika maonyesho hayo, imeweza kujenga majengo ya kudumu pamoja na vipando vya mazao mbalimbali ambayo yamekuwa yakisaidia kutoa elimu kwa wakulima.

"JKT tumekuwa mfano bora katika maonyesho yote yanayofanyika katika kanda mbalimbali nchini, tumewekeza vya kutosha na vipando vyetu vya mazao mbalimbali ni vya kudumu kwa muda wa mwaka mzima, hivyo kwa kutumia vijana wetu wenye utaalamu tunawapatia elimu wakulima," alisema.

Naye Mkurugenzi wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema wamepokea ushindi huo wa nafasi ya kwanza kitaifa kwa taasisi za utafiti nchini kwa furaha kubwa kwa kuwa zipo taasisi nyingi za utafiti nchini.

Dk. Mkamilo alisema katika maonyesho mengine yaliyofanyika katika viwanja vingine ikiwamo Nyamuongoro mkoani Mwanza, Tabora na Nzuguni Dodoma pia TARI imepata ushindi wa kwanza kwa taasisi za utafiti.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi hiyo ya TARI, Dk. Yohana Budeba, alisema wamefurahishwa na kuonekana kuwa taasisi wanayoisimamia inatekeleza majukumu yake kwa vitendo katika utafiti ukilinganisha na zingine.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (wa pili kushoto), akimkabidhi kombe Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Kanda ya Ziwa, Ayubu Kalufya, baada ya kuibuka washindi wa pili wa huduma za mawasiliano, katika kilele cha maonyesho ya wakulima (Nanenane) kitaifa mkoani Simiyu, wikiendi. Kushoto ni Katibu Tawala wa mkoa huo, Mariam Mmbaga. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Watoto 9 wapata ujauzito likizo corona

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI tisa wa shule za msingi zilizopo Halmashauri ya Kahama Mjini mkoani Shinyanga, wamepata ujauzito wakati wa likizo ya mlipuko wa homa kali ya mapafu (corona) na kusababisha kukatisha masomo na kushindwa kutimiza ndoto zao.

Wanafunzi hao wawili walipata ujauzito kabla ya kufungwa kwa shule zote nchini na saba wakipata ujauzito baada ya kufungwa kwa shule hizo, huku bodi za shule zikiwasimamisha masomo na kuendelea na kesi zilizofunguliwa mahakamani dhidi ya wahusika wa mimba hizo.

Salma Mwenda, Ofisa Elimu Afya shule za msingi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, aliyabainisha hayo jana wakati wa warsha ya kuongeza uelewa walimu wa afya kuhusu kujikinga na kujilinda dhidi ya Covid-19 na mapambano ya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi iliyoandaliwa na Huheso Foundation kwa ufadhili wa The Foundation for Civil Society (FCS).

Alisema upatikanaji wa ujauzito kwa wanafunzi wa kike wa shule za msingi na sekondari unachangiwa na ushiriki mdogo wa wazazi kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao baada ya mwanafunzi kutoka shule na kwapatia uhuru wa muda wa kuingia nyumbani bila kujua wametoka wapi na kufanya nini.

"Tunawanafunzi tisa waliopata ujauzito na wameshasimamishwa masomo na bodi zetu za shule, idadi hii inaweza kuongezeka hivi karibu kutokana na walimu kuendelea na uhakiki na kuwarodhesha majina wanafunzi wenye ujauzito shule zote 80 za msingi," alisema Mwenda.

Naye Ofisa Afya wa Halmashauri, Basil Gervas, alisema wananchi wameanza kupuuza agizo la unawaji wa mikono na uvaaji wa barakoa na kuwataka walimu kuendelea kuwahimiza wanafunzi kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka kabla na baada ya kuingia darasani.

Mratibu wa mradi wa baki salama kutoka Shirika lisilo la kiserikali la Huheso Foundation, Gerald Muheto, alisema mradi huo unatekelezwa kwenye kata tano za Zongomela, Nyasubi, Kahama Mjini, Malunga na Majengo.

Akizungumza kwa niaba ya walimu, mwalimu wa Shule ya Msingi Kahama "A", Rahel Lobozi alisema, wanapata shida ya kuwahimiza wanafunzi kuendelea kunawa mikono na kuvaa barakoa wakati wakiwa shuleni kutokana na kuona jamii inayowazunguka kutoendelea kuchukua tahadhari.

# RC Ndikilo atekeleza agizo la PM

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amemwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesai kwa kushirikiana na viongozi wa wafugaji wa mkoa huo, kukamata wafugaji wanaodaiwa kulisha mifugo yao katika mashamba ya wakulima.

Mashamba hayo yapo Kata ya Ruvu Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Vijijini.

Ndikilo pia alitoa siku saba kwa wafugaji wote walio ndani ya kata hiyo, kupeleka mifugo yao katika Ranchi ya Ruvu ili kuondoa kero kwa wakulima ambao wamedai kushindwa kulima ekari 1,000 badala yake wamelima ekari 30 kutokana na kuhofia mifugo kuharibu mazao yao.

Alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akisikiliza kero za wakazi wa kata ya Ruvu katika mkutano uliofanyika Kijiji cha Minazi Mikinda ikiwa ni hatua ya kutekeleza agizo la Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, alilolitoa Agosti 7, 2020 akimtaka kufika katika eneo hilo na kuongea na wananchi.

**Malalamiko mengi yaliyotolewa na wananchi wa kata hiyo ni kuhusiana na baadhi ya wafugaji ambao wamekuwa wakisababisha uharibifu kwenye mashamba ya wakulima na kukaidi kulipa fidia.**

Ndikilo alisema malalamiko mengi yaliyotolewa na wananchi wa kata hiyo ni kuhusiana na baadhi ya wafugaji ambao wamekuwa wakisababisha uharibifu kwenye mashamba ya wakulima na kukaidi kulipa fidia, huku viongozi wa kata hiyo nao wakishindwa kutumia sheria kudhibiti hali hiyo.

Ndikilo alipiga marufuku ya mifugo kuonekana katika bonde la Mto Ruvu, na kwamba wakulima watakaoshuhudia hali hiyo wanatakiwa kutoa taarifa kwake pamoja na Mkuu wa Wilaya hiyo, Martine Ntemo, ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

"Kuanzia leo mifugo haitakuwa katika bonde la Mto Ruvu sio mchana wala usiku, utaratibu utafanywa na mkoa kwa kushirikiana na chama cha wafugaji mifugo itengewe vitalu kulingana na idadi iliyopo katika Ranchi ya Ruvu, hii itaondoa kero kwa wakulima kwa kuwa wengi wao wamekuwa na hofu ya kulima kwa kushindwa kumudu kupambana na wafugaji," alisema.

Alisema Ranchi ya Ruvu NARCO imetenga zaidi ya ekari 20 kwa ajili ya mifugo, wafugaji wapeleke mifugo yao huko ambapo watalipa gharama nafuu kwa kuwa kufanya hivyo tutapunguza migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo inaonekana kukwamisha maendeleo na kuleta hofu ya kuibuka njaa.

Awali akizungumza katika mkutano huo, Majala Chuma, mkazi wa kata ya Ruvu, alisema, kumekuwapo na utaratibu wa baadhi ya viongozi kuwasajili wafugaji bila kupitia vikao halali, jambo linalosababisha ongezeko la mifugo katika kata hiyo ambayo inalishwa kwenye mashamba ya wakulima.

Ndikilo alifanya mkutano wa siku moja kutekeleza agizo la Waziri Mkuu alilolitoa alipokuwa Kijiji Cha Minazi Mikinda akikagua ujenzi wa reli ya kisasa, ambapo wakazi wa kijiji hicho walijitokeza kwa wingi na kuanza kumwelezea kero zao, ikiwamo suala la mifugo iliyokithiri inayokwamisha kilimo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Simon Karikari (mwenye tai), akipata maelezo kuhusu bidhaa mbalimbali zinazouzwa katika banda la kampuni hiyo, wakati wa kilele cha maonyesho ya wakulima (Nanenane), katika viwanja vya Nyakabindi, mkoani Simiyu, wikiendi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Athari kupandisha mifugo ya ukoo mmoja

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

UPANDISHAJI wa mifugo ya ukoo mmoja unaweza kusababisha athari kadhaa, ikiwamo maumbile ya jinsia mbili.

Hayo yalisemwa na ofisa mifugo wa Kata ya Gera Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, Enock Mehova baada ya Nipashe kuona mbuzi wa kisasa mwenye jinsia mbili katika Kata ya Kanyigo wilayani humo.

Mehova alisema sababu ya kutokea kwa maumbile hayo mara nyingi ni kutokana na kupandisha mbuzi wa ukoo mmoja, hivyo kusababisha matatizo hayo.

"Ninaposemea ukoo mmoja namaanisha baba na mama upande wake mbuzi anakuwa amerithi mababu zao huko wakija kupandisha yanatokea madhara kwa mtoto anapozaliwa," alisema Mehova.

Alisema mbuzi wa aina hiyo anakuwa na faida ya nyama na mbolea kwani hana uwezo wa kuzaa wala kuzalisha.

"Ukimwangalia hivi ni vigumu kutambua kwa haraka kwani hakuna matiti ya kunyonyeshea, pia mfuko wa uzazi haujakamilika," alisema Mehova.

Aidha, alisema maumbile ya mbuzi huyo hayajakamilika ambayo yangefanya kuonyesha.

Aliongeza kuwa akiwa ndani ya kundi anasaidia mfugaji kutambua jike ambalo limeingia kwenye joto.

"Anasaidia sana akiwa kwenye kundi analazimisha kupanda majike wengine na ukiingiza dume humu wanapigana hadi asubuhi," alisema Mehova.

Mfugaji wa mbuzi huyo, Joas Ishengoma, alisema tangu amezaliwa mwaka 2018, hadi sasa hajawahi kuzaa.

Ishengoma alisema mifugo mingine ambayo imezaliwa kipindi kimoja imeshazalishwa mara mbili.

"Nilishangaa ndipo nikawachukua wataalamu wa mifugo kuja kuangalia na imeshaingia kwenye joto," alisema Mehova.

Alisema walifika ndani ya banda ndiyo walitambua kuwa ana jinsia mbili.

# Serikali yapewa tano kufyeka ushuru wa kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** BARIADI

WAKULIMA nchini sasa wana fursa na manufaa makubwa katika sekta ya kilimo kutokana na mageuzi yaliyofanywa hivi karibuni katika maeneo ya kodi, ushuru na tozo mbalimbali.

Hayo yalibainishwa na wakulima na wadau wa kilimo waliohudhuria maonyesho ya Nanenane kitaifa kwenye Viwanja vya Nyakabindi wilayani Bariadi mkoani Simiyu walipotembelea banda la maonyesho la Policy Analysis Group (PAG).

Katika kipindi chote cha wiki nzima ya Nanenane, Policy Analysis Group ilitumia fursa hiyo kujadiliana na wadau mbalimbali kuhusu mageuzi ya sera zinazoihusu sekta ya kilimo nchini.

"Maonyesho ya Nanenane yametupa fursa kubwa. Siyo tu kukutana na washiriki na wadau wa kilimo, bali pia kuongeza uelewa kuhusu mageuzi ya sera ya hivi karibuni na kupata mrejesho kutoka kwa wadau wetu kuhusu mambo ya sera ambayo bado hayajafanyiwa kazi," alisema Mratibu wa Programu (TAP) kutoka Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) ambaye ni mmoja wa wajumbe wa PAG.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TAHA, Jacqueline Mkindi, alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, kuna marekebisho zaidi ya 100 katika kodi, tozo na ushuru yamefanyika katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuendeleza na kukuza uchumi wa wakulima nchini.


"Kama wajumbe wa PAG, tunaamini kuwa ushirikiano na ubia wa dhati kati yetu ndiyo nguzo ya kuleta mabadiliko zaidi katika kukuza na kuendeleza uchumi wa wakulima wa Tanzania," alisema.

Mkuu wa Kanda ya Afrika Mashariki wa AGRA, Nuhu Hatibu, alisema ubia ni mkakati bora katika kuharakisha uboreshaji wa sera nzuri na mabadiliko jumuishi ya kilimo nchini, akibainisha kuwa umoja na ushirikiano huu ndani ya PAG una nguvu ya kupeleka mbele gurudumu la maendeleo jumuishi.

Policy Analysis Group ni jukwaa linalojumuisha sekta mbalimbali kwa lengo la kuendeleza uratibu na ubia katika majadiliano na uchambuzi wa sera, ili kuchangia na kuharakisha utekelezaji wa mageuzi ya sera katika sekta ya kilimo nchini.

"Policy Analysis Group inafanya kazi kwa karibu na sekta ya kilimo katika kusaidia na kuharakisha maboresho ya sera ili kuweka mazingira wezeshi, kuongeza kipato cha mkulima, kuboresha lishe, usalama wa chakula na maendeleo ya viwanda," alisema Mwenyekiti wa Policy Analysis Group, Audax Rukonge.

Nipashe
TESA
Jumanne Agosti 11, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 12

## Miaka mitano yaondoka ikiacha wanafunzi milioni 12 darasani



Ukurasa 14

**MLIPUKO BEIRUT: Amonium naitreti ni nini, ni hatari kwa namna gani?**



Ukurasa 13

Hifadhi wahitaji zinapofaulu, zinachochea kukiuka wajibu

ELIMU NA SABATO KASIKA

# Itapendeza zaidi kuwapo vioski vya maziwa shuleni



Wanafunzi wakigawiwa maziwa katika mojawapo ya shule nchini. **PICHA: MTANDAO**

KARIBU shule nyingi za msingi na sekondari hasa za mijini, pembeni mwake kuna wafanyabiashara ambao hutoa huduma kama za kurudufu (fotokopi), kuchapa, kuuza vitafunwa, kukaanga chips, wapo pia wanaouza pipi na mahitaji mengine yanayowalenga wanafunzi.

Biashara hizo zinafanyika ili kusaidia wanafunzi kupunguza makali ya njaa wawapo shuleni, hasa kutokana na ukweli kwamba, baadhi hazijaanza utaratibu wa kutoa chakula shuleni.

Wapo baadhi ya watu walifikia hadi kufungua baa na nyumba za kulala wageni karibu na maeneo ya shule, lakini serikali ikaingilia kati kwa kuagiza kuvunjwa kwa baa na nyumba hizo.

Mfano ni Dar es Salaam, ambapo mwaka 2017, aliyekuwa mkuu wa mkoa huo, Paul Makonda , aliagiza kuvunjwa kwa baa na nyumba hizo ili kuepusha wanafunzi na hatari ya kujiingiza kwenye mambo ya ngono na uhalifu mwingine.

Agizo hilo lilisaidia kutuliza hali ya hewa na kubakia biashara ya ndogo zikiwamo za vyakula ambazo hadi sasa zinaendelea katika maeneo mbalimbali ya shule jijini humo.

Wakati biashara hizo zikiendelea, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anashauri sasa kila shule kuwa na kibanda cha kuuza maziwa ili kusaidia wanafunzi kuboresha afya zao.

Anasema, hajapiga marufuku uuzwaji wa vyakula vingine, bali anashauri kila shule hasa za bweni kuwa na kibanda cha maziwa ili fedha ambazo wanafunzi hupewa na wazazi kununulia vyakula, wanunue pia maziwa wapate lishe bora.

Ndivyo anavyosema waziri huyo mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya Siku ya Lishe, iliyofanyika kitaifa jijini Dodoma.

Anasema atamwandikia barua Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, kumshauri kuhusu mpango huo.

Anasema, ni muhimu kuwe na mazingira wezeshi ya kusaidia kuwapo kwa vioski au vibanda vya kuuzia maziwa shuleni na kwamba siyo lazima wale wanaofanya biashara shuleni kwa sasa ndiyo wauze maziwa hayo.

Waziri Ummy anasema, lengo lake ni kupendekeza kuanzia Septemba mosi mwaka huu, kila shule ya msingi na sekondari iwe na kibanda cha maziwa kwa ajili ya wanafunzi kupata lishe.

"Kuanzisha vioski au vibanda vya kuuza maziwa shuleni hasa zile za kutwa, kutawezesha wanafunzi kuboresha afya zao na pia kupanua soko la bidhaa za maziwa na kuongeza kipato kwa jamii," anasema Ummy.

Aidha, akizungumzia utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO), anasema, unaonyesha kuwa kila mtu anatakiwa kunywa nusu lita ya maziwa kila siku hivyo kufikisha 180 kwa mwaka.

"Lakini kwa sasa wastani kila mtu anakunywa lita 40 za maziwa kwa mwaka sawa na vijiko 10 vya chai kwa siku, ipo haja ya kuhimiza jamii kunywa maziwa na kwa shule ni muhimu kila moja kuwa na kibanda vya maziwa," anasema.

Anasema, jambo la muhimu ni kuweka mazingira wezeshi ili kila vioski au katika vibanda 10 vya biashara katika kila shule, kinakuwapo kimoja cha kuuza maziwa, hivyo utaratibu wa kuwapata watakaowekeza ufanyike ili watafutwe watu wa kuwekeza katika biashara hiyo.

"Kama nilivyosema, siyo vibaya wakitafutwa wajasiriamali ili kuhakikisha kama kuna vioski 10, kimoja kiwe cha kuuza maziwa kwa ajili ya wanafunzi. Msisitizo uwe ni kunywa maziwa ili kuboresha afya za watoto wetu," anasema.

Sambamba na hilo, Waziri Ummy, anaitaka Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), kuharakisha mwongozo vyenye virutubisho kwa watoto.

Anasema, mwongozo huo unaandaliwa na taasisi hiyo kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) kupitia ufadhili wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP).

**APIGA MARUFUKU**

Pamoja na wazo la kutaka kuanzisha vibanda vya maziwa shuleni, waziri anapiga marufuku utoaji wa vidonge vya Asidi ya Foliki kwa wanafunzi au wasichana waliopevuka badala yake viendelee kutolewa kwa wajawazito na wanawake walio katika umri wa kuzaa.

Anasema, fedha zinazotolewa na wadau wa maendeleo kwa ajili ya kununua vidonge hivyo, zitumike kuanzisha bustani shuleni ili kuzalisha vyakula vinavyotoa madini hayo.

"Fedha hizo pia zinaweza kupelekwa kwa vijana ili waanzishe miradi ya bustani za mboga kwa ajili ya kuzalisha mazao yanayozalisha asidi hiyo badala ya kutoa vidonge kwa wanafunzi," anasema.

Waziri Ummy, anafafanua kuwa kuanzisha bustani, vijana watapata ajira na wataongeza kipato lakini pia watakuwa wamezalisha vyakula vyenye asidi ya foliki ili kusaidia wanafunzi badala ya vidonge hivyo.

"Hivyo kuna mambo mawili ya muhimu hapa, kuanzia unywaji wa maziwa shuleni, ambao nitamwandikia barua Waziri wa Elimu Profesa Ndalichako, ili kutoa pendekezo kuanzia Septemba mosi mwaka huu kila shule iwe na kibanda cha maziwa na pia suala la vidonge," anasema.

**KUWEKEZA LISHE**

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe, Dk. Germana Leyna, anasema, kuna haja ya kuhamasisha sekta mbalimbali zikiwamo binafsi kuwekeza katika lishe.

Dk. Leyna anasema, hatua hiyo ni muhimu hata kwa viwanda, ili uwekezaji wao uwe pia katika utengenezaji wa vifaa vya kupimia hali ya lishe nchini, lengo likiwa ni kuboresha afya za Watanzania.

"Katika maadhmisho ya siku hii ya leo, tunaona tuwe sehemu ya kuhamasisha sekta mbalimbali zikiwamo za binafsi hasa viwanda kuwekeza katika lishe kwa kutengeneza vifaa vya kupimia hali ya lishe," anasema Dk. Leyna.

ELIMU

NA AUGUSTA NJOJI, DODOMA

# Miaka mitano yaondoka ikiacha wanafunzi milioni 12 darasani

MIAKA mitano ya serikali ya awamu ya tano imeanzisha utekelezaji wa sera ya utoaji wa elimu bila malipo kuanzia elimumsingi hadi kidato cha nne, ilipoingia madarakani mwishoni mwa 2015.

Sera hiyo inayotokana na tamko namba 3.1.5 la sera ya elimu na mafunzo ya mwaka2014, na waraka wa elimu namba 5 wa mwaka 2015 unaohusu elimu bila malipo, utekelezaji wake unatajwa kuwa ni miongoni mwa mipango madhubuti iliyoleta mafanikio kwenye sekta ya elimu.

Ilianza kutekelezwa baada ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, kuingia madarakani mwishoni mwa mwaka 2015, na kutoa fursa kwa wanafunzi kusoma na kupata elimu bila mzazi au mlezi kulipa ada wala michango ya fedha iliyokuwa ikitozwa kabla ya waraka huo.

Katika utekelezaji wa sera hii, serikali ya awamu tano ilianza na utengenezaji wa madawati kwa nchi nzima ambao ulisimamiwa na wakuu wa wilaya na mikoa.

Baada ya kutengeneza madawati, serikali ilianza ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa shule za msingi na sekondari, sambamba na uboreshaji wa miundombinu kwa shule za msingi na sekondari na kuajiri walimu.

Utekelezaji wake umeleta mwamko mkubwa sana kwa wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao shule tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Kuanzia Januari 2016, idadi kubwa ya wanafunzi wanaoandikishwa kuanza darasa la kwanza na wanaojiunga na kidato cha kwanza kwa shule za umma imeendelea kuongezeka kwa kasi mwaka hadi mwaka.



Katika miaka mitano ya awamu ya kwanza, serikali ya JPM imeongeza idadi ya wanafunzi shuleni pamoja na kuboresha miundombinu ya kusomesha. **PICHA: AUGUSTA NJOJI.**

**MILIONI 10 DARASANI**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali zaMitaa(TAMISEMI) Selemani Jafo, anasema utekelezaji wa sera hiyo umeongeza idadi ya wanafunzi walioandikishwa kutoka 10,201,972 mwaka 2015 hadi 12,034,599 mwaka 2020, kwa shule za msingi.

"Uondoaji wa ada na michango isiyo ya lazima umewawezesha wanafunzi wengi zaidi hasa wanaotoka katika familia duni kupata fursa ya kwenda shule na kusoma bila vikwazo "anasema Waziri. Aidha, kwa upande wa shule ya sekondari anasema idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka 1,806,955 mwaka 2016 hadi 2,023,457 mwaka 2020.

Anasema wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wameongezeka kutoka asilimia 60 mwaka 2015 hadi asilimia 100 mwaka 2020.

"Rais Magufuli wakati anaomba kura alikusudia matokeo haya chanya na tunamshukuru sana kwa kuwa mpango huu umewawezesha wanafunzi wengi zaidi hasa wanaotoka katika familia duni kupata fursa hii na kusoma,"anasema Jaffo.

Aidha, anabainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Desemba, 2015 hadi Juni, 2020, serikali imetumia Sh. trilioni 1.09 kugharamia elimu bila malipo.

"Kati ya fedha hizo kiasi Sh. bilioni 502.2 zimetumika shule za msingi na bilioni 593.9 kwa shule sekondari kwa ajili ya chakula kwa wanafunzi wa bweni wa kutwa kwa shule zenye wanafunzi wenye uhitaji maalum, ruzuku ya uendeshaji ,fidia ya ada na posho ya madaraka kwa maofisa elimu kata na wakuu wa shule za msingi na sekondari,"anasema.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Joseph Nyamhanga, anasema mpango huo ni moja ya mikakati waliyoiweka katika kufikia malengo hayo kwa kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi ili kufanya uwe fanisi zaidi na wenye kuzingatia mahitaji ya kila mwanafunzi.

Anataja mikakati mingine kuwa ni kujenga na kukarabati miundombinu ya shule, kuendelea kutoa ajira kwa walimu,kutoa mafunzo kazini kwa walimu na viongozi wa elimu.

> "Miundombinu iliyojengwa ni pamoja na vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, mabwalo ya chakula, vyoo, maabara, maktaba, mabweni na majengo ya utawala," anasema Mweli.

Aidha kuhamasisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji na ujifunzaji,kuboresha mifumo ya takwimu za elimu,kuimarisha usimamizi, kuimarisha utoaji wa elimu maalum, kutoa mafunzo nje ya mfumo rasmi na kuimarisha michezo shuleni.

**UKARABATI MKUBWA**

Akizungumzia mafanikio mengine katika sekta ya elimu yaliyopatikana chini ya usimamizi wa TAMISEMI kwa kipindi cha miaka mitano, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli, anasema kipindi cha kuanzia Desemba, 2015 hadi Juni, 2020 kimeshuhudia Sh. bilioni 501.78 zikitumika kujenga, kukamilisha na kukarabati miundombinu ya elimu shule za msingi na sekondari.

"Miundombinu iliyojengwa ni pamoja na vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, mabwalo ya chakula, vyoo, maabara, maktaba, mabweni na majengo ya utawala," anasema Mweli.

Anaongeza kuwa juhudi hizo zimetokana na utekelezaji wa mipango mbalimbali ukiwamo Programu Endelevu ya Usambazaji wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (SRWSS), anasema Mweli.

Kadhalika, anasema hadi kufikia Juni 2020 ujenzi wa shule mpya za msingi 905 ulikuwa umekamilika hivyo kuongeza idadi yake kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 17,804 mwaka 2020.

"Vyumba vya madarasa 17,215 vimejengwa na na sasa vimeongezeka kutoka 108,504 mwaka 2016 hadi 125,719 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia13.7 ambapo ujenzi wa vyumba 3,049 unaendelea na ukikamilika idadi ya vyumba vya madarasa kwa shule za msingi utafikia 128,768,"anasema Mweli.

Aidha madawati yameongezwa kutoka 3,024,311 mwaka 2015 hadi kufikia 8,095,207 sawa na ongezeko la zaidi ya asilimia 200.

"Upande wa shule za sekondari serikali imejenga shule mpya 228 na hivyo kuongezeka kutoka shule 4,708 mwaka 2016 hadi 5,330 mwaka 2020, vyumba 227 vya maabara za masomo ya sayansi vimekamilishwa kwa gharama ya Sh. bilioni 2.63,ujenzi ambao umeongeza idadi ya vyumba vya maabara kutoka 4,237 mwaka 2015 hadi 4,464 mwaka 2020,"anasema.

Mweli anasema uwekezaji na maboresho yaliyofanyika katika sekta ya elimu kwa shule za msingi na sekondari umeongeza kiwango cha ufaulu katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi kutoka asilimia 67.84 mwaka 2015 hadi asilimia 81.50 mwaka 2019.

TEKNOLOJIA

**NA MICHAEL ENEZA**

# Hifadhi wahitaji zinapofaulu, zinachochea kukiuka wajibu

YAKO maeneo magumu katika mustakabali wa maadili au dhana inayoyahusu, kwa mfano watu kwa kawaida wanatoa sala au dua ya kufaulu kwa biashara zao, ila kwa mfano kuna mtengeneza majeneza, sala yake nayo isikilizwe au itupiliwe mbali?

Ni katika hisia kama hiyo unaweza kuangalia miradi ya kusaidia watoto yatima ambayo miaka iliyopita ilikuwa inasikika sana, lakini siyo rahisi kusikia wakitajwa siku hizi. Hapo pia kuna swali, kama imekuwa hali ya kawaida kwa watoto kupata misaada kama hiyo kwa hiyo jitihada kama hizo si habari kwa maana ya kuchangamsha watu, au wamechokwa?

Juhudi za kuangalia watoto yatima zinaendana na mustakabali mpana wa jamii kwa wakati uliopo, hasa unapozingatia kuwa vituo vya kulea watoto yatima vilikuwa vinaazishwa na watu binafsi kwa misaada ya mashirika ya nje yanayojali watoto. Kulikuwa na manung'uniko ya hapa na pale kuwa wanaoanzisha vituo hivyo wanavitumia kujinufaisha, bila kufafanua kama walikuwa wanavuna ziada ya mahitaji halisi au ya msingi ya watoto wanaowaangalia, au ni kwa kukiuka wajibu huo. Jitihada hizo zinafanyika katika jamii ambayo maadili yake kwanza yana mashaka, na ndiyo sababu ya awali ya watoto kuishia mitaani.

Yako maeneo kadhaa ya lengo la kuwalea watoto walioachwa mitaani, na kisaikolojia yanaweza kufaulu kwa viwango tofauti. Eneo la kwanza ni hifadhi ya chakula na malazi, na hata elimu, ambayo kwa jumla ilielekea kufanikiwa, ila kukawapo matatizo katika eneo jingine, la maadili kwa upande mmoja kwani watoto hao hawawezi kulindwa vya kutosha wasivurugwe na jamii inayowazunguka. Hali hiyo pia inaleta utata katika hatua nyingine ya malezi, kuwa wakifikia umri haiwi rahisi kuingia mitaani na kutafuta maisha katika hali ya kawaida, kwani umri wa miaka 18 haumwondolei kijana kuitegemea familia yake.

Siku hizi siyo rahisi kusikia kuna kibaka aliyekamatwa, au hata jambazi, ambaye alilelewa katika kituo kimoja au kingine, wakati nyakazi za awali (miaka ya kwanza ya karne mpya) jambo hilo lilikuwa linasikika mara kwa mara. Hiyo inaonyesha kuwa kwa vile vijana kama hao tayari wanafahamika katika vituo vya malezi ya watoto yatima, wanaweza kuingiza mitandao ya uhalifu na kuanza 'kuopoa' vijana hasa pale wanapohitajiwa kuondoka katika vituo vya malezi kwa umri. Kuweka pamoja vijana wadogo na waliofikia umri katika mazingira ya kulea, siyo kusoma na kurudi nyumbani, bila shaka kunaleta hatari.



Watoto ni tunu kama watalelewa na kutunzwa na familia. **PICHA: MTANDAO.**

Ila hatari kubwa zaidi ni jamii ambayo kwa sehemu isiyo ndogo ina maadili potofu ya kuona watoto kama mzigo na siyo faraja katika maisha, watu kama hao wakijua kuna mahali wanaweza kupeleka watoto wakapata huduma zote, watawawahisha watoto wao.

Lengo ni kupata urahisi wa kuwakimbia wanawake na hao watoto, kwani wajibu wa kumjali mwanamke ni ili aweze kumudu mahitaji ya watoto, na siyo hasa mahitaji yake yeye mwenyewe pale ambapo mzazi mwenzie hamhitaji kihisia.

Ni eneo mojawapo la uharibifu wa maadili siyo kutokana na 'utandawazi' ila uhuru, kuvunjika kwa jamii ya awali, kuitegemea sheria badala ya kuwapo nguvu ya wazazi, wakuu wa jadi, hata nyumba za ibada zenye mamlaka kijamii.

> Ni eneo mojawapo la uharibifu wa maadili siyo kutokana na 'utandawazi' ila uhuru, kuvunjika kwa jamii ya awali, kuitegemea sheria badala ya kuwapo nguvu ya wazazi, wakuu wa jadi, hata nyumba za ibada zenye mamlaka kijamii.

Ukiangalia machapisho mtandaoni kuhusu kulea watoto wa mitaani, unapata picha kuwa wengi tu wanafaulu katika maisha, kwa mfano binti mmoja ng'ambo alionyeshwa amekuwa muuguzi. Siyo rahisi kufuatilia hali hiyo huku Tanzania kwani uwezekano wa watoto wanaofikia umri wa miaka 18 kuendelea kuwa na uhusiano na vituo vya malezi siyo mkubwa, na labda siyo wote ambao wanakaa katika vituo hivyo hadi wafikie umri wa kuhitajiwa au kutazamiwa kujitegemea.

Dhana ya watoto kutupwa mitaani na kupata msaada katika vituo vya kulea na kuelimisha watoto kwa misaada hasa ya mashirika ya nje inaweza kulinganishwa na hali ngumu ya 'usafirishaji watu' kimataifa ambako vijana wengi wanatafuta njia za kuondoka nchi za Afrika kuhamia Ulaya. Sababu ni kama zile za watoto wadogo, wanaokimbia nyumbani hasa kutokana na mateso ya mama wa kambo au shangazi pale mama yake amekufa au kuna sababu zilizomtenga naye, au amekimbia unyumba wa awali kwa mateso, akaacha mtoto au watoto.

Kwa kanuni za jamii yetu hatuna dhana ya haki za watoto ila ofisini; nyumbani ziko koo, na watoto wanaotambuliwa na ukoo ni wale waliozaliwa na wanaume wa ukoo huo, siyo waletwe kutoka kwingine.

Ndiyo maana mkakati wa kuleta watoto waliosahaulika mitaani ni kama kuokota majani chini ya mti ambao unaendelea kukauka, kwani utakuwa unapukutisha majani kila kukicha. Tatizo siyo kwamba watu watazaa watoto wasio na mpango wa kuwalea kwa sababu kuna vituo hivyo, ila pale ambako unyumba unaanza kwenda kombo, uhakika wa watoto kulelewa bila wazazi kuwa pamoja unapokuwepo, ni wazi utaharakisha kufumuka kwa uhusiano huu au unyumba kutokana na vivutio nje.Ni pamoja na jitihada za kisaikolojia na nyinginezo, kumvuta mzazi au mume pengine mwenye mke na watoto awaache ili kujihusisha na nyumba ndogo.

SAYANSI

**NA MWANDISHI WETU**

## MLIPUKO BEIRUT:

# Amonium naitreti ni nini, ni hatari kwa namna gani?

TAIFA la Lebanon limepitia mengi kama vita, mizozo na majanga. Lakini kilichotokea Jumanne wiki iliyopita katika bandari ya Beirut kilishinda chochote kile ambacho raia wa nchi hiyo wangefikiria.

Mlipuko katika bandari hiyo uliharibu sehemu kubwa ya mji huo mkuu na kubakiza vifusi na kuwafanya watu takribani 2,000 kupoteza maisha wengine maelfu kuwa walemavu na 300,000 kukosa makazi na kuondoa matumaini ya maisha bora ambayo waliyafurahia hasa vijana na watoto wadogo.

Kwa siku kadhaa sasa, shughuli ya kutafuta waliopotea katika mkasa huo inaendelea bila ya msaada wa serikali na hakuna mwanasiasa aliyewajibika. Badala yake, serikali imekuwa ikipongeza ujasiri wa raia wa taifa hilo.

Ni wazi kwamba hakuna aliye madarakani anayejihisi kuhusika na ukweli kwamba kemikali ya ammonia naitreti yenye kiwango kikubwa cha kulipuka ilihifadhiwa katika bandari ya Beirut kwa muda wa miaka sita karibu na maeneo ambayo watu wanafanya kazi na kuishi katikati mwa mji huo.



Rais wa Lebanon, Michel Aoun, akitafakari makubwa yaliyoikumba nchi yake.

Bandari ilivyogeuka kuwa kifusi baada ya mlipuko wa Jumanne iliyopita. PICHA: MTANDAO.

Badala yake wamewakamata baadhi ya maofisa wakuu wa bandari. Kama hali inavyokuwa kila kunapokuwa na matatizo nchini Lebanon, hakuna aliye madarakani anayelaumiwa.

Wiki iliyopita ilianza vibaya huko Lebanon baada ya takribani tani 3,000 za kemikali ya amoniam naitreti zilizohifadhiwa miaka sita iliyopita katika ghala kulipuka na kusababisha balaa kubwa katika eneo la bandari ya mji kuu wa nchi ya Lebanon. Mkasa huo uliotokea Jumanne, unaacha maswali mengi hivyo ni vyema kufahamu 'ammonium nitrate' ni nini na kwa nini inaweza kuwa kemikali hatari?

'Ammonium nitrate' ni kemikali iliyo na umbo la mabonge meupe ambayo hutengenezwa viwandani.

Matumizi yake makubwa ni pamoja na kutengeneza mbolea ya chumvichumvi, lakini pia inatumika kwa ajili ya kutengeneza vilipuzi kwa ajili ya migodi. Baruti zinazotumiwa kulipua miamba na majabali zinazotokana na kemikali hiyo.

Kemikali hii hutengenezwa duniani kote na ni rahisi kununuliwa.

Lakini, utunzaji wake unaweza kuwa tatizo na imekuwa chanzo cha ajali kadhaa za viwandani miaka ya nyuma.

### HATARI ILIYOMO

Amoniam naitretini hatari kwa kiasi gani? Ni swali ambalo linamgusa pengine kila aliyefuatilia mkasa wa Beiruti.

Kemikali hiyo ilivyo inaelezwa kuwa ni salama, anasema profesa wa kemia Andrea Sella kutoka shule ya sayansi ya Chuo Kikuu cha London.

Hata hivyo, ukiwa na kiasi kikubwa cha kemikali hiyo kwa muda mrefu huanza kuoza.

"Tatizo ni kwamba kadiri muda unavyokwenda kemikali huanza kufyonza unyevu na hatimaye hubadilika kuwa mawe makubwa," anasema. Hatua hii hufanya kemikali hiyo kuwa hatari zaidi, anajiongeza, kwa kuwa inamaanisha kuwa ukitokea kitu cha kuistua itasambaa kirahisi zaidi.

Kadiri inapoachwa muda mrefu, kuna uwezekano zaidi wa kuchafuliwa na vitu kama mafuta, anasema ofisa wa intelijensia ya jeshi Philip Ingram alipozungumza na BBC.

Inapotokea hali hiyo inaweza kusababisha athari kwenye kemikali. "Hutengeneza joto lake yenyewe na ikianza kufanya hivyo, inaendelea kutengeneza joto hilo kwa muda," Ingram anasema.

"Hali hiyo baadaye inaweza kusababisha mlipuko mkubwa kama tulioushuhudia kwenye video ya kutisha kutoka mji wa Beirut."

> "Tatizo ni kwamba kadiri muda unavyokwenda kemikali huanza kufyonza unyevu na hatimaye hubadilika kuwa mawe makubwa," anasema. Hatua hii hufanya kemikali hiyo kuwa hatari zaidi, anajiongeza, kwa kuwa inamaanisha kuwa ukitokea kitu cha kuistua itasambaa kirahisi zaidi.

### NINI KILITOKEA

Swali nini kilichotokea mjini Beirut linajibiwa kuwa mlipuko huo ulitokea muda mfupi saa 12 asubuhi Jumanne.

Mwandishi wa BBC aliyekuwa katika eneo hilo aliripoti miili ya watu waliokuwa wameuawa na uharibifu mkubwa unaoweza kuifunga bandari hiyo ya Beirut kwa muda.

Vyombo vya habari viliwaonyesha watu wakiwa wamenasa chini ya vifusi.

Shuhuda mmoja alielezea mlipuko huo kuwa mkubwa hali inayoweza kusababisha watu kuwa viziwi, huku picha ya video ikionyesha magari na nyumba zilizoharibiwa

Kwa namna gani gesi zinazotengenezwa huwa hatari? Kemikali ya amoniam naitreti inapolipuka, hutengeneza gesi ya sumu ikiwemo 'nitrogen oxide' na gesi ya amonia

Moshi wa rangi ya chungwa husababishwa na gesi ya nitrojen daiyoksaid, ambayo huambatana na uchafuzi wa hali ya hewa.

"Kama hakuna upepo wa kutosha, huwa hatari zaidi kwa watu walio karibu na eneo la tukio," anasema Prof Sella.

### KUZALISHA MABOMU

Kwa mlipuko huo, ammoniam naitret imekuwa ikitumika na majeshi duniani kote kama vilipuzi

Pia imekuwa ikitumika katika matukio kadhaa ya kigaidi, ikiwamo tukio la mabomu la mji wa Oklahoma mwaka 1995. Katika tukio hilo, Timothy McVeigh alitumia tani mbili za amoniam naitreti kutengeneza bomu lililoharibu jengo la serikali na kusababisha vifo vya watu 168.

Tukio kama hili lilishawahi kutokea sehemu nyingine hapo kabla kwa mfano mwaka 1921, takribani tani 4,500 za ammoniam naitrete zilisababisha mlipuko katika vinu vya Oppau, Ujerumani na kusababisha vifo ya watu 500.

Ajali mbaya ya kiwandani katika historia ya Marekani ilitokea mwaka 1947 mjini Galveston Bay, jimbo la Texas. Takribani watu 581 walipoteza maisha baada ya tani zaidi ya 2,000 zilipolipuka kwenye meli ambayo ilitia nanga bandarini.

Tukio la karibuni ni la mlipuko wa kemikali hiyo na nyingine ambapo watu 173 walipoteza maisha katika bandari ya Tianjin Kaskazini mwa China mwaka 2015.





# Watanzania wahimizwa matumizi nishati mbadala

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kutumia nishati mbadala ili kusaidai taifa kuondokana na janga la uharibifu wa mazingira unaosababishwa na ukataji miti kwa ajili ya matumizi ya nishati ya mkaa, hali inayochangia mabadiliko ya tabia nchi.

Hayo yalibainishwa juzi jijini Dodoma na Meneja Masoko wa Kampuni ya Premium Active Tanzania Ltd, inayozalisha nishati mbadala ya mkaa mweupe Aristotle Nikitas, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Nikitas, alisema matumizi ya mkaa mweusi ambao unatumika hivi sasa katika maeneo mengi ya nchi umekuwa ndiyo chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira.

**Mkaa unaotumika hivi sasa umeharibu uoto wa asili kwa kiasi kikubwa na kusababisha kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya tabia nchi.**

Alisema, umefika wakati sasa Watanzania wakabadili mitazamo yao na kuanza kutumia nishati mbadala ambazo hazina madhara kwa afya zao pamoja na mazingira.

"Huu mkaa mweupe ambao leo tunautangaza hapa Dodoma ni nishati ambayo ni rafiki wa mazingira kwa kuwa tunatengeneza kwa kutumia majani maalumu ambayo tunayapanda wenyewe na wala hatuharibu mazingira kabisa," alisema Nikitas.

Alisema, mkaa unaotumika hivi sasa umeharibu uoto wa asili kwa kiasi kikubwa na kusababisha kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya tabia nchi.

"Mkaa mweupe huu ni rafiki wa mazingira, lakini afya ya watumiaji kwani mkaa ule mweusi pamoja na kuharibu mazingira, pia umekuwa si rafiki kwa afya ya watumiaji una hewa ya carbon kwa asilimia 80, hii ni hatari sana kwa afya," alisema.

Kadhalika, alisema mkaa mweupe ni salama kwa afya ya mtumiaji kwa kuwa una kiasi cha asilimia tisa ya hewa ya carbon hivyo ni salama zaidi.

"Hivi sasa tumekuwa tukitoa elimu katika shule na maeneo mbalimbali juu ya matumizi ya mkaa huu mweupe ili jamii iondokane na matumizi ya mkaa mweusi ambao si salama kwa afya zao pamoja mazingira," alisema.

Vilevile, alisema kutokana na wafanyabiashara ya mkaa kuangalia maslahi yao binafsi wanakata kila mti bila kujali aina ya sumu zilizomo kwenye mti husika.

"Kila mti hua una sumu yake, hivyo wafanyabiashara hawana muda wa kuangalia mti gani wa kukata, wanakata kila mti hivyo watumiaji ndio wanaweza kuwa katika hatari ya kupata madhara mbalimbali ya kiafya,"



Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya NMB, wakishiriki kwenye mkutano wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi ya Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO), uliofanyika jijini Dodoma juzi. Benki hiyo, ilishirikishwa kama taasisi ya kifedha inayotoa huduma za kifedha kwa wanafunzi na wafanyakazi wa vyuo vya juu nchini. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wafugaji watakiwa kufuga kwa tija

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amewataka wafugaji nchini kubadilika na kuacha kufunga makundi makubwa ya mifugo isiyokuwa na tija bali wawe na itakayo wawezesha kujikwamua kiuchumi.

Simbachawene, aliyasema hayo juzi wakati alipokuwa akikagua ng'ombe wa maonyesho katika banda la Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwenye maonyesho ya wakulima Nanenane, yaliyofanyika katika viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma.

Alisema, ufugaji wa sasa unasikitisha kwa kuwa wafugaji wengi bado wanafuga kienyeji hali ambayo inasababisha washindwe kujikwamua kiuchumi.

Alisema, wafugaji wengi wanafurahi kuona wanamiliki makundi makubwa ya mifugo ambayo haina tija kwao zaidi ya kuowaongezea gharama za utunzaji pamoja na migogoro na wakulima.

"Unakuta mfugaji anamiliki kundi la ng'ombe 500, lakini hakuna hata mmoja anayefaa kwa maziwa wala kwa nyama, lakini mfugaji amekonda na mifugo yake pia imekonda balaa," alisema Simbachawene.

Pia, alisema wafugaji kuendelea kufunga makundi makubwa ya mifugo kunachangia migogoro baina yao na wakulima kutokana na kutokuwapo kwa malisho ya kutosha.

"Tunatakiwa kufuga kisasa kiasi kidogo cha mifugo ambacho kitasaidia wafugaji wetu kunufaika na mifugo hiyo na kiasi cha malisho tulichonacho ili kuondokana na migogoro ya wakulima na wafugaji ya kila mara, lakini hii itasaidia taifa kupata mapato kupitia sekta ya mifugo," alisema.

Hata hivyo Simbachawene, alisema maonyesho ya Nanenane, yanatakiwa kutumika kutoa elimu kwa wafugaji ili kubadilika katika mitazamo yao na kunufaika na mifugo yao.

Alisema ni wakati sasa wafugaji nchini kubadilika na kuacha kufuga kimazoea ili kwenda sambamba na jitihada za serikali kujikwamua wananchi wake kiuchumi kwa kuanzisha viwanda mbalimbali vinavyotumia malighafi za mifugo.

# Wanafunzi wenye ulemavu watoa kilio kwa serikali

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WANAFUNZI wenye ulemavu wanaosoma shule za msingi mkoani Dodoma wameiomba serikali kuwachukulia hatua kali za kisheria wazazi na walezi wanaowanyima haki za msingi watoto wao kwa kuwaficha majumbani.

Mwanafunzi Deo Kasimbu wa Shule ya Msingi Nkuhungu alisema hayo, kwenye hafla fupi ya kupokea misaada mbalimbali ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona, kwa ajili ya watoto wenye ulemavu iliyotolewa na mradi wa Elimu Jumuishi kitengo cha kanisa la FPCT Wilaya ya Dodoma na Bahi.

Akizungumza kwa niaba ya watoto wenye ulemavu, aliiomba serikali kuhakikisha wale wote wanaowanyima haki za msingi kisheria ikiwamo kuwaficha majumbani, unyanyasaji na unyanyapaa, wasifumbiwe macho bali wachukuliwe hatua kali kwa wanaobainika.

Alisema bado kuna changamoto nyingi kwa watoto wenye ulemavu kutokana na tabia ya kufichwa majumbani kwa imani kuwa ni mkosi, badala ya kupelekwa shule ili na wao wapate haki zao za msingi kama vile elimu na afya.

"Jamii lazima itambue kuwa kitendo cha kuwaficha majumbani watoto wenye ulemavu, ni kuongeza umaskini zaidi kwenye familia husika tofauti na wangepelekwa shuleni na kupata elimu na ujuzi ambao utasaidia kuondoa umaskini," alisema.

Akizungumzia misaada hiyo, mwanafunzi huyo aliwataka wahisani wengine kuelekeza macho yao kwa watoto hao wenye ulemavu, kutokana na changamoto walizonazo ambazo baadhi yake wanaweza kushindwa kufikia ndoto zao.

Kwa upande wake Mratibu wa Mradi huo, Wilaya ya Bahi na Dodoma, Jane Mgidange, alisema serikali, taasisi, mashirika na watu binafsi wana jukumu kubwa la kuhakikisha watoto wenye ulemavu wanatatuliwa changamoto zinazowakabili.

Alisema, pamoja na serikali kutangaza kuondoka kwa maambukizi ya corona hapa nchini, lakini bado wamepewa angalizo la kuendelea kujikinga, hivyo kwa upande wa mradi wameona kuwasaidie watoto wenye ulemavu.

"Mradi pamoja na kutoa elimu kwa watu wenye ulemavu kuhusina na suala zima la afya na elimu, pia tunaomba taasisi, mashirika na watu binafsi kuhakikisha tunaisaidia serikali katika kuwaletea maendeleo kwa makundi maalumu katika kuinua uchumi wao," alisema.

**Bado kuna changamoto nyingi kwa watoto wenye ulemavu kutokana na tabia ya kufichwa majumbani kwa imani kuwa ni mkosi, badala ya kupelekwa shule na wao wapate haki zao za msingi kama vile elimu na afya.**





# Wafanyabiashara wagomea amri ya DC

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

ZAIDI ya wajasiriamali 300 wa soko la Utyego, Kata ya Ubaruku, Mbarali mkoani Mbeya, wamegoma kutii amri ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, ya kuwataka waondoke katika eneo hilo wakidai kuwa ni eneo lao halali.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi, wajasiriamali hao walidai kuwa mkuu huyo wa wilaya amewapa siku tatu wavunje vibanda vyao na kuondoka na kwamba baada ya muda huo kwisha kama watakuwa hawajaondoka kwa hiari wataondolewa kwa nguvu.

Mmoja wa wananchi hao, Joachim Thabiti, alisema awali walikuwa wanafanya shughuli zao kwenye eneo ambalo lilikuwa na mgogoro kati ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na serikali, ambapo CCM ilishinda na kusababisha wajasiriamali waondolewe.

**Kabla Ofisi ya Mkurugenzi haijaushughulikia muhtasari huo, wananchi walianza kufanya shughuli zao ikiwamo ujenzi wa vibanda na kuweka meza.**

Alisema waliondolewa tangu Machi, mwaka huu, hivyo tangu wakati huo walikuwa hawana eneo la kufanyia shughuli zao mpaka walipoamua kukaa Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Utyego ulioamua kubadili matumizi ya eneo hilo ambalo lilikuwa kwa ajili ya michezo na kuwa la biashara.

Thabiti alisema mhutasari wa mkutano huo ulipelekwa hata katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, lakini wanashangaa Mkuu wa Wilaya ambaye anawataka waondoke huku akidai kuwa vibanda ambavyo wamejenga ni uchafu.

"Ametwambia tuondoke hapa, lakini hajatuambia twende wapi. Sisi hapa hili ni eneo letu kama kijiji na tulikubaliana kubadili matumizi baada ya kukosa eneo la kufanyia shughuli zetu baada ya kufukuzwa kwenye eneo la CCM hakuwahi kututetea," alisema Thabiti.

Naye Monica Msamba, alisema hawana eneo lingine ndani ya kijiji hicho la kufanyia biashara na kwamba wanaendesha maisha yao kwa kutegemea biashara hiyo, hivyo hawako tayari kuondoka kwenye eneo hilo.

Alisema hata kama Mkuu wa Mkoa ataamua kutumia nguvu kuwaondoa wao hawataondoka na wataendelea kufanya shughuli zao kwenye eneo hilo.

"Chama kimetunyanyasa kwenye eneo lake na serikali inakuja kutuondoa kwenye eneo letu? Tunamwomba Rais (John) Magufuli atusaidie maana maisha yetu yanakuwa magumu na sisi hatufungamani na chama chochote," alisema Msamba.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Dickson Shija, alikiri kusimamia Mkutano wa Kijiji ambao ulifanyika Julai 30 na kukubaliana kubadili matumizi ya eneo ambalo lilikuwa la michezo na kuwa soko na kwamba aliupeleka muhtasari katika Ofisi ya Mkurugenzi.

Alisema kabla Ofisi ya Mkurugenzi haijaushughulikia muhtasari huo, wananchi walianza kufanya shughuli zao ikiwamo ujenzi wa vibanda na kuweka meza.

Alikiri kupokea amri ya Mkuu wa Wilaya ya kuwataka wajasiriamali hao waondoke na kwamba yeye hawezi kupinga amri hiyo na badala yake ataendelea kufuata taratibu za uongozi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alikiri wananchi hao kufuata taratibu za kubadili matumizi ya eneo hilo na kuwa la biashara na kwamba anachopinga ni wananchi hao kuanza kufanya biashara kabla hawajajenga miundombinu muhimu.

Alisema katika eneo hilo hakuna choo wala ghuba la kuhifadhia taka na hivyo sio sahihi kuwaruhusu waendelee kufanya shughuli zao hapo na kwamba msimamo wake uko pale pale wa kuwataka waondoke.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Antony Sanga, akinywa maji kwenye chanzo cha maji cha Nyerere, katika Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, Mkoa wa Mbeya, alipofanya ziara ya kukagua miradi ya maji mkoani humo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Chokaa ya rutuba kuwafikia wakulima

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TANI 100 za chokaa yenye rutuba kwa ajili ya afya ya udongo zinatarajiwa kutolewa kwa wakulima 66,000 katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa na Arusha ili kuongeza uzalishaji wa mazao.

Ofisa Habari wa Shirika la One Acre Fund, Dorcas Tinga, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe walivyojipanga kuwasaidia wakulima katika msimu ujao wa kilimo na kwamba chokaa hiyo itasaidia kuongeza uzalishaji kutoka magunia 10 kwa ekari hadi 20.

Tinga alisema bidhaa hiyo ya chokaa itamsaidia mkulima kupata mavuno mengi kwa sababu ina madini aina ya Acid ambayo yanaongezeka kwenye udongo kutokana na matumizi ya mara kwa mara ya mbolea na kuathiri afya ya udongo.

Alisema mkulima akitumia bidhaa ya chokaa itasaidia kushusha madini ya (Acid) na kuongeza madini ya calcium pamoja na magnesium ambayo yatasaidia mkulima kupata mavuno mengi.

"Tayari bidhaa iko sokoni na itaanza kutumika katika msimu ujao wa kilimo na kuwahamasisha wakulima ambao ardhi yao haizalishi kwa wingi mazao kutumia ili kupata faida," alisema Tinga.

Aliongeza kuwa malengo ya shirika hilo ni kuwawezesha wakulima kwa kuwapatia mikopo ya pembejeo za kilimo kwa sharti la kujiunga kwenye vikundi vya kuanzia watu watano hadi 16.

Baadhi ya wakulima walidai kwa sasa ardhi haina rutuba kutokana na matumizi ya mbolea pamoja na wataalamu kutotoa elimu sahihi ya kilimo hali inayosababisha kutopata mavuno mengi.

Miongoni mwao Joseph Martin alisema imani yao chokaa hiyo inaweza kuwa mwarobaini wa kuongeza rutuba kwenye udongo na kuchochea uzalishaji.

## Wadaiwa kuwa na mwamko mdogo matumizi mradi maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wametajwa kuwa na mwamko mdogo wa kuomba kuunganishiwa huduma ya maji ya bomba.

Hali hiyo inaelezwa kuwa imesababisha maji ya mradi wa maji wa Shongo kukosa watumiaji licha ya kukamilika kwa asilimia 98. Mradi huo ni ule ambao Rais John Magufuli, aliiagiza Wizara ya Maji kuukamilisha Mei 25, mwaka jana, alipokuwa kwenye ziara ya kikazi mkoani hapa baada ya wananchi wa mji huo kulalamikia kukosa huduma hiyo kwa muda mrefu.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Antony Sanga, katika mradi huo, Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya- WSSA), Ndele Mengo, alisema mradi huo unazalisha kati ya lita milioni 8.5 mpaka milioni 10 kwa siku.

Alisema mahitaji ya wakazi wote wa Mji wa Mbalizi ni lita milioni 7.1 lakini mpaka sasa maji yanayotumika ni chini ya lita 4,000,000 hali ambayo inasababisha kiwango kikubwa cha maji ya mradi huo kutotumika. Alisema kwa sasa wanaendelea kupeleka huduma hiyo katika Bonde la Songwe ambalo pia lilikuwa linalengwa kunufaika na mradi huo pamoja na kuanza kuondoa baadhi ya mabomba ya zamani ambayo yamechakaa na kuweka mapya.

Aidha, aliiagiza mamlaka hiyo kuongeza kasi ya kusajili wateja wanaohitaji kuunganishiwa huduma hiyo ili mradi uwe na tija kwa wananchi wa mji huo ambao waliomba mradi huo kutoka kwa Rais Magufuli.

# Ataka kukamilika jengo la mafunzo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Kamishna Chuo cha Mafunzo Zanzibar (Magereza), Haji Hamdu Omar, amemwagiza mkuu wa kitengo cha ujenzi kuhakikisha wanalimaliza jengo la ofisi ya 'aluminium' kwa wakati uliopangwa.

Kamishna Haji alisema hayo wakati akiweka jiwe la msingi la jengo hilo lililoko makao makuu ya chuo hicho Kilimani.

Alisema chuo hicho kimeanzisha kitengo cha kutengeneza vifaa mbalimbali vya 'aluminium' ili kuzalisha na kujiletea maendeleo ndani ya chuo kama alivyoagiza Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, la kuzitaka taasisi za kiserikali na binafsi kuzalisha mali ili kujiletea maendeleo.

Naibu huyo alisema chuo hicho pia kinatoa fursa kwa wananchi wa kawaida na taasisi binafsi kwenda kununua vifaa vinavyotengenezwa na chuo hicho.

Akizungumzia maagizo ya kutotazamwa wafungwa na mahabusu baada ya kuwapo kwa maradhi ya corona, alisema hivi sasa chuo kimepunguza masharti hayo na kuruhusu wananchi ambao wanakwenda kuwaona na kuwapelekea chakula jamaa zao.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wananchi kufuata masharti yaliyowekwa na Wizara ya Afya na madaktari wa chuo hicho na bado serikali haijatangaza rasmi kwamba maradhi ya corona kuwa yameondoka moja kwa moja.

"Ni lazima sisi chuo na taasisi zingine tuendelee kuchukua tahadhari juu ya maradhi haya," alisema.

Hata hivyo aliwataka maofisa na askari na familia zao kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na maradhi hayo ambayo bado yanaendelea kuzisumbua nchi jirani.

Naye Mkuu wa Ujenzi, Mrakibu Juma Makame Mataka, aliahidi kuhakikisha jengo hilo linamalizika mwishoni mwa mwezi huu kama ilivyopangwa ili kuleta maendeleo kwa chuo na taifa kwa ujumla. Zaidi ya Sh. milioni 14 zinatarajiwa kutumika.

**Chuo hicho pia kinatoa fursa kwa wananchi wa kawaida na taasisi binafsi kwenda kununua vifaa vinavyotengenezwa na chuo hicho.**

# Balozi Iddi asisitiza amani kwa maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema ustawi wa sekta ya kilimo unahitaji uwepo wa amani na utulivu ili wananchi wanaoitegemea wapate maendeleo yatakayochangia pato la taifa.

Amesema bila amani na utulivu, hakuna mwananchi atakayethubutu kwenda shambani, baharini au msituni kutafuta riziki na hatimaye atashindwa kupata mahitaji yake muhimu ikiwamo chakula, elimu na matibabu.

Balozi Iddi alisema hayo juzi wakati akifunga Maonyesho ya Tatu ya Kilimo yaliyokuwa yakifanyika Chamanangwe, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Makamu wa Pili aliupongeza uongozi wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kusimamia na kufanikisha shughuli hiyo muhimu ya maonyesho ya kilimo, maarufu kama Nanenane.

**Ni jukumu la kila mwananchi kuhakikisha anatumia haki yake ya kidemokrasia bila kushawishiwa na kusababisha vurugu zisizo na maslahi kwa wengi.**

Alisema umahiri wa uongozi huo umesababisha wananchi wengi kujitokeza kwa wingi na kushiriki kikamilifu katika maadhimisho hayo na kupata fursa ya kuuza bidhaa wanazozitengeneza wenyewe.

Balozi Iddi alisema vijana mbalimbali wajasiriamali wakiwamo pia kinamama wamejifunza mambo tofauti ya kukuza mitaji yao iliyosaidia kujiongezea kipato katika kipindi kidogo cha maonyesho.

Alisema mambo hayo yanatimiza dhamira ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya kuwa maonyesho ya kilimo ni njia mojawapo ya kuwafikia wananchi wengi kwa muda mfupi katika kutoa elimu na kuonyesha teknolojia mpya za uzalishaji.

Kuhusu uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu, alisema ni jukumu la kila mwananchi kuhakikisha anatumia haki yake ya kidemokrasia bila kushawishiwa na kusababisha vurugu zisizo na maslahi kwa wengi.

Alisema maisha bado yataendelea kuwapo baada ya uchaguzi, hivyo Watanzania wanapaswa kuelewa kwamba wote ni ndugu wanaowajibika kuepuka mifarakano na wazingatie upendo na kufuata sheria za nchi.

Naye Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, alivishukuru vyombo vya ulinzi na halmashauri kwa umakini wao uliowezesha kufanikiwa kwa maonyesho hayo.

Ujumbe wa mwaka huu wa Maonyesho ya Tatu ya Kilimo ulikuwa "Tudumishe Amani na Utulivu kwa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Zanzibar".



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd na ujumbe wake wakiangalia miche ya minazi iliyooteshwa kwenye kitalu kilichopo ndani ya eneo la maonyesho ya kilimo ya Nanenane Chamanangwe, Mkoa wa Kaskazini Pemba. **PICHA: OMPR – ZNZ**

# Matatani tuhuma za kujifanya askari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi linawashikilia watu wawili wanaodaiwa kujishughulisha na vitendo vya utapeli dhidi ya wananchi na kujifanya maofisa wa jeshi hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Awadh Juma Haji, alithibitisha kukamatwa kwa watu hao alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mwembe Madema, mjini hapa.

Awadhi aliwataja watuhumiwa hao ni Ali Said Masoud (47) mkazi wa Chuini ambaye aliwahi kuwa askari polisi mwenye namba F.2941 cheo cha Konstebo ambaye alikuwa akifanya kazi kituo cha polisi Ng'ambo Wilaya ya Mjini, lakini alifukuzwa kazi mwaka 2012 kwa kosa la ujambazi.

Alimtaja mtuhumiwa mwingine kuwa ni Salum Khatib Mkwende (43) mkazi wa Miembeni ambaye aliwahi kuwa askari wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ambaye alifukuzwa kazi mwaka 2008 kwa kosa la utoro jeshini.

Kamanda alisema katika kutekeleza matukio ya utapeli, watuhumiwa hao hupita kwenye nyumba za wageni hasa maeneo ya Fuoni na kuwavizia wanawake wanaotoka kwenye nyumba hizo kisha kuwatapeli fedha kwa kujitambulisha kuwa wao ni askari polisi.

Alisema watuhumiwa hao huwalazimisha wananchi wawapatie fedha na wasipotoa huwatishia kuwafikisha kwenye vituo vya polisi kwa kujihusisha na biashara ya ukahaba.

Kamanda Awadhi alisema watuhumiwa hao kwa sasa si waajiriwa tena kwenye serikali bali hufanya ubabaishaji na vitendo vya kihalifu kwa kujinadi kuwa wao ni askari.

Sambamba na hayo, aliwataka wanawake kuondoa nidhamu ya woga pindi anapokuja mtu kujitambulisha kuwa ni askari, anapaswa ahoji na kuuliza kosa lake la msingi ili kuepusha kurubuniwa kirahisi.

Aidha, Kamanda aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama ili kupunguza urahisi wa kutapeliwa na wasisite kukagua vitambulisho vyao vya kazi kubaini ukweli na kujiridhisha.

HABARI KIMATAIFA

# Watoa mabilioni kuichangia Lebanon

**BEIRUT,** Lebanon

VIONGOZI mbalimbali duniani wameahidi kuichangia Lebanon zaidi ya Euro milioni 250 baada ya nchi hiyo kukumbwa na milipuko miwili mikubwa kwenye Bandari ya Mji wa Beirut.

Viongozi na mashirika ya kimataifa wametoa ahadi hiyo kwa ajili ya kuisaidiia Lebanon baada ya nchi hiyo kukumbwa na maafa yaliyosababishwa na mlipuko mkubwa.

Hata hivyo, viongozi na mashirika hayo yameeleza kwamba, fedha hizo zinazokusudiwa kwa ajili ya ujenzi mpya wa mji mkuu wa nchi hiyo Beirut, hazitatolewa mpaka viongozi wa Lebanon watakapohakikisha kwamba watafanya mageuzi ya kisiasa na kiuchumi ambayo wananchi wanayataka.

**Kwa kuzingatia msingi wa kibinadamu tunapaswa kusaidia. Vipi nchi inaweza kuhimili maafa kama haya. Na kwa hivyo tutawasaidia kwa kiwango kikubwa.**

Viongozi walioshiriki kwenye mkutano huo walikuwa ni Rais wa Marekani, Donald Trump, Mfalme Abdullah wa pili wa Jordan, Rais Abdel Fattah el-Sisi wa Misri, viongozi wa Umoja wa Ulaya na wajumbe kutoka China. Mkutano huo uliongozwa na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron.

Washiriki zaidi ya 30 kwenye mkutano huo wa kimataifa waliahidi msaada kwa ajili ya kufanyika uchunguzi wa kuaminika.

Akizungmzia juu ya msaada kwa Lebanon, Rais Trump alisema:

"Kwa kuzingatia msingi wa kibinadamu tunapaswa kusaidia. Vipi nchi inaweza kuhimili maafa kama haya. Na kwa hivyo tutawasaidia kwa kiwango kikubwa. Tayari ndege zetu kubwa tatu zimepeleka mahitaji ya dawa. Hali ni mbaya sana lakini tutawasaidia."

Rais wa Lebanon wanataka uchunguzi ufanyike juu ya mlipuko uliotokea wiki iliyopita uliosababisha vifo vya watu wapatao 160. Watu wengine zaidi ya 6,000 walijeruhiwa kutokana na mlipuko huo.

**MAWAZIRI, WABUNGE WAJIUZULU**

***Wakati huo huo***, mawaziri kadhaa wamejiuzulu ikiwa ni ishara namna serikali ya Lebanon inavyosambaratika.

Waziri wa Mazingira, Demanios Kattar, ambaye amejizulu alisema serikali ya Lebanon imekwama. Alisema serikali hiyo haina uwezo wa kufanya chochote.

Waziri wa Mawasiliano wa Lebanon, Manal Abdel Samad alikuwa waziri wa kwanza kujiuzulu akisema kuna haja ya mabadiliko.

Nchini Lebanon endapo idadi ya mawaziri wanaojiuzulu itafikia saba kati ya 20, Baraza la Mawaziri litalazimika kujiuzulu na nafasi yake itachukuliwa na serikali ya mpito.

Wakati huohuo, maandamano yameendelea kwenye mitaa ya mjini Beirut ya watu wanaotaka mageuzi. Mamia ya watu wanawalaumu viongozi wa serikali kwa usimamizi mbovu na kwa ufisadi.

Nayo Iran imesema maafa ya Lebanon hayapaswi kugeuzwa mtaji wa kisiasa na imeitaka Marekani iondoe vikwazo ilivyoweka dhidi ya Lebanon ikiwa nchi hiyo inayo dhamira ya kweli ya kuisaidia. **DW**



Viongozi wa Muungano Mkuu wa Upinzani nchini Kenya (NASA) wakiwa katika picha ya pamoja. Kiongozi wa Chama cha ODM, Raila Odinga, amekiri kuwa muungano huo umesambaratika. **PICHA: REUTERS**

## Raila Odinga asema NASA imesambaratika

**NAIROBI,** Kenya

KIONGOZI wa chama cha upinzani cha ODM nchini Kenya, Raila Odinga, amekiri kuwa muungano mkuu wa upinzani nchini humo, NASA umesambaratika.

Odinga alidai kuwa muungano hufa usiposhinda kwenye uchaguzi na hivyo ndivyo muungano huo ulivyosambaratika baada ya uchaguzi mkuu uliopita.

Hata hivyo, kiongozi mwenza kwenye muungano huo, Musalia Mudavadi, ametofautiana na kauli ya Raila.

Nyufa kwenye Muungano Mkuu wa upinzani NASA, zilianza kudhihirika pindi tu, kiongozi wake Raila Odinga alipozika tofauti zake za kisiasa na Rais wa nchi hiyo, Uhuru Kenyatta, katika kile kilichokuja kufahamika kuwa salamu za heri, baada ya uchaguzi wenye utata mwaka 2017.

Baadaye kiongozi mwenza wa Chama cha Wiper, Kalonzo Musyoka, alipewa wadhifa wa kuwa mjumbe maalum kwenye mzozo wa Sudan Kusini na hata akasaini mkataba wa ushirikiano na chama tawala cha Jubilee.

Kauli ya Raila inatia kikomo mahusiano ya kisiasa ambayo amekuwa nayo na viongozi wenza wa Muungano huo kama vile, Musalia Mudavadi wa Chama cha Amani National Congress na Moses Wetangula, wa Ford Kenya.

Viongozi hao walimuunga mkono Raila kwenye uchaguzi mkuu uliopita mwaka 2017.

Matamshi ya kiongozi wa ODM yanajiri huku wito wa kuwa na mwakilishi mmoja kwenye kiti cha urais ukiongezeka. **DW**

## Wasiojulikana wafanya shambulio, waua watu 8

**NIAMEY,** Niger

WATU wanane wakiwamo raia sita wa Ufaransa na wawili wa Niger wameuawa na watu wenye silaha nchini Niger.

Taarifa zaidi zinaeleza kwua wauaji hao ambao bado hawajafahamika walikuja kwa pikipiki katika eneo la Kouré, Kusini Magharibi mwa nchi, linalojulikana kama malisho hifadhi ya mwisho ya twiga huko Afrika Magharibi.

Paris imethibitisha kwamba Wafaransa wameuawa katika shambulio hilo, lililotokea juzi, bila kutoa idadi kamili.

Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, pia alizungumza kwa simu na mwenzake wa Niger, Mahamadou Issoufou, Ikulu ya Elysee ilieleza.

Agosti 9, katika mji wa Kouré, mashariki mwa mji mkuu wa Niger, watu wenye silaha waliwapiga risasi watu wanane, ikiwa ni pamoja na raia wawili kutoka Niger na Wafaransa sita.

Habari hiyo ilitolewa na Shirika la Habari la AFP na kuthibitishwa kwa RFI na Tidjani Ibrahim Katiella, Gavana wa Mkoa wa Tillabéri.

"Watu wanane waliuawa, Wafaransa sita na raia wawili kutoka Niger. Majambazi wenye silaha waliokuwa katika magari ndio walihusika na vifo vya raia hao katika eneo la kitalii la Kouré. Eneo hili ni hifadhi ya Twiga, Twiga wa mwisho katika Afrika Magharibi," alisema Gavana huyo na kuongeza:

"Tumeanzisha uchunguzi na tumeanza pia kuwasaka majambazi hao katika eneo hilo. Tuna huzuni mkubwa, na ni tukio la kusikitisha kwa kweli. Katika siku za hivi karibuni, tulikuwa katika hali ya utulivu, tumeshtushwa na tukio hilo, inauma kwa kweli," alisema Gavana wa Mkoa wa Tillabér

Rais wa Ufaransa na mwenzake wa Niger wamebaini kwamba watafanya msako ili kubaini mazingira ya mauaji hayo. Wameapa kuendelea na vita dhidi ya makundi ya kigaidi huko Sahel.

Baraza la ulinzi litakutana leo chini ya uenyekiti wa Rais wa Ufaransa kulingana na taarifa zitakuwa zimetolewa jana na viongozi wa Niger na Ufaransa.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Niger ilieleza kuwa operesheni ya kusaka majambazi hao inaendelea, ambapo Jeshi la Barkhane linashiriki. **RFI**

# MARTINEZ AFURAHIA KUBAKI INTER



**MILAN,** Italia

LAURATO Martinez "anafuraha sana" pale Inter Milan huku akihusishwa na miamba wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Barcelona, kwa mujibu wa wakala wake, Beto Yaque.

Martinez amekuwa akitajwa anaondoka Inter kwenda Barca mwishoni mwa msimu, ingawa klabu hiyo ya Italia mara kwa mara imesisitiza haina mpango wa kumuuza mshambuliaji wao huyo.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, kipengele cha mkataba wake cha kutakiwa kuuzwa kwa euro milioni 111 kilimalizika Julai na Yaque ameondoa uwezekano wa uhamisho wake kutoka kwenye dimba la San Siro kwenda Camp Nou.

"Uhamisho wa Lautaro upo zaidi kwenye vyombo vya habari kuliko maisha halisi," alisema Yaque akiiambia La Figura de la Cancha. "Lautaro ana miaka mitatu kwenye mkataba wake na Inter na ana furaha sana pale alipo.

"Alikuwa na msimu mzuri sana, hivyo kwa sasa siwezi kuzungumza kuhusu uwezekano wa kuondoka." Yaque aliongeza: "Kamwe sijahitaji kumpa ushauri na sihitaji kufanya hivyo sasa. Mara zote amekuwa ni mchezaji aliyepevuka."

Martinez amefunga mabao 14 kwenye Serie A wakati kikosi hicho cha kocha, Antonio Conte, Inter kikimaliza nafasi ya pili kwa kupitwa pointi moja na mabingwa Juventus kwa msimu wa 2019-20. Raia huyo wa Argentina amefunga mabao 19 katika mashindano yote.

# Lampard kuisuka upya Chelsea

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard ameelezea kuijenga upya timu yake baada ya kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora kwa kichapo cha uwiano wa mabao 7-1 kutoka kwa Bayern Munich.

Lampard ambaye aliweka rekodi ya ufungaji mabao Chelsea, alifurahi wakati wake kama mchezaji kwa kubeba mataji ya Ligi Kuu ya England, na Ligi ya Mbingwa Ulaya, amebainisha kwamba wanahitaji kuijenga upya timu ili kufikia mafanikio hayo.

"Kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita tulikuwa na wachezaji, timu yenye (Eden) Hazard, (Diego) Costa, (Petr) Cech, (John) Terry na (Didier) Drogba," alisema Lampard akinukuliwa na BT Sport baada ya kichapo cha mabao 4-1 kutoka kwa Bayern, Jumamosi.

"Kushindana kwenye Ligi Kuu mwaka hadi mwaka, kufuzu fainali na nusu fainali mara kwa mara. Tunajua kwamba hicho si kitu kwa sasa... lazima tufanyie kazi kwa kujenga kikosi cha Chelsea."

Lampard, ambaye aliiongoza Chelsea kumaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu na kutinga fainali ya Kombe la FA katika msimu wake wa kwanza, amesema ataangalia namna ya kuimarisha kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao.

Chelsea tayari imeshanunua washambuliaji, Hakim Ziyech na Timo Werner.

"Tutaliangalia hilo kwa makini sana, kwa sababu hiyo ni kazi yetu," aliongeza Lampard.





# *Zola aishangaa Juve kumpa ukocha Pirlo*

**TURIN,** Italia

GIANFRANCO Zola amesema "alishangazwa" na maamuzi ya Juventus kumteua Andrea Pirlo kuwa kocha wao mkuu baada ya kufukuzwa kwa Maurizio Sarri.

Pirlo mwenye umri wa miaka 41, aliteuliwa na Juve kuwa kocha Mkuu Jumamosi baada ya mabingwa hao wa Serie A kumfukuza Sarri kwa kutolewa na Lyon kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16.

Kiungo huyo wa zamani wa Juve, Pirlo, ambaye hivi karibuni aliteuliwa kuwa kocha wa kikosi cha Juventus chini ya umri wa miaka 23, sasa ataanza kuonja ladha ya kuwa kocha wa kikosi cha wakubwa cha 'Bianconeri' hao.

Zola ambaye alifanya kazi kama msaidizi wa Sarri pale Chelsea msimu wa 2018-19, ameiambia Sky Sport Italia: "Nitakuwa naongopa kama nikisema sikushangazwa na hili.

"Ni kazi inayovutia na kama akifanya vizuri, yatakuwa mafanikio makubwa zaidi kwa klabu hiyo. Si kazi rahisi, ingawa kama Juventus wanao uwezo wa kushinda kwa namna yoyote.

"Hili ni jambo la kutia moyo kwa klabu na hasa kwa ubora wa mtu husika, lakini Pirlo atahitaji sapoti ili kusonga mbele. Si rahisi, lakini nafikiri anaweza kupata mafanikio."

Pirlo aliondoka Juve mwaka 2015 baada ya Bianconeri hao ambao walikuwa wanatafuta kushinda mataji matatu msimu huo, kufungwa mabao 3-1 na Barcelona katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alitumia miaka miwili akiwa kule kwenye Ligi Kuu ya Marekani (MLS), akiwa na New York City kabla ya kustaafu soka.

## HABARI MICHEZO



# ALABA BADO SHIDA BAYERN

**MUNICH,** Ujerumani

DAVID Alaba amekataa kujibu maswali juu ya majaliwa yake na amesema Bayern Munich inasafiri kwenda Lisbon kwenye mchezo wao wa robo fainali dhidi ya Barcelona, huku wakiwa hawana cha kuhofia.

Mlinzi huyo wa kimataifa wa Austria, Alaba bado hajasaini mkataba mpya pale kwenye dimba la Allianz Arena, huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwakani.

Manchester City, inayonolewa na kocha wa zamani wa Bayern, Pep Guardiola, Paris Saint-Germain, Chelsea, Barcelona na Real Madrid ni miongoni mwa timu zinazowania saini ya Alaba.

Bayern wamekuwa na matumaini makubwa ya kumbakiza Alaba, ingawa mchezaji huyo kwa sasa hataki kuzungumzia hayo, kwani akili yake ameielekeza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Akili yangu kwa sasa ipo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ndio maana sitaki kuzungumza lolote kuhusu majaliwa yangu," alisema.

Alaba alikuwa sehemu ya kikosi cha Bayern kilichoifunga Chelsea mabao 4-1 Jumamosi na kupata ushindi wa uwiano wa mabao 7-1 katika mchezo wao wa pili wa hatua ya 16-bora.

## Pirlo: Ni heshima kuwa kocha wa Juventus

**TURIN,** Italia

ANDREA Pirlo amelezea kujivunia kwake kuteuliwa kuwa kocha mkuu wa Juventus wakati akizungumza kwa mara ya kwanza hadharani baada ya uteuzi huo Jumamosi.

Mabingwa wa Serie A, Juve waliamua kufanya mabadiliko katika benchi lao la ufundi baada ya kutolewa na Lyon kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora, Ijumaa.

Kocha, Maurizio Sarri alifukuzwa siku iliyofuata, huku Pirlo akipewa mikoba hiyo akipandishwa kutoka timu ya vijana chini ya umri wa miaka 23, kwa mkataba wa miaka miwili.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Italia mwaka 2006, alitumia mtandao wa kijamii kutoa ya moyoni akisema: "Kwa hakika kabisa kutoka ndani ya moyo wangu nimepewa heshima kubwa kuwa kocha wa Juventus na nawashukuru kwa imani yao kwangu.

"Hakika hii ni nafasi ya kuvutia sana!"

Aliongeza: "Ni kazi kubwa na ngumu, lakini naamini ushirikiano nitakaoupata utawezesha mimi na Juventus kusonga mbele."

Pirlo sasa atakuwa mpinzani mkuu wa kocha wa Inter Milan, Antonio Conte, ambaye ni kocha wake wa zamani hapo Juve na Italia.





## Pedro aelekea Roma

**LONDON** England

PREDO amethibitisha kuondoka Chelsea baada ya "miaka mitano ya kuvutia" akiwa na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England.

Mshambuliaji huyo wa Hispania, amemaliza mkataba wake na Blues hao na sasa ameripotiwa kwamba anaelekea nchini Italia, kujiunga na miamba wa Serie A, AS Roma kwa mkataba wa miaka miwili. Mchezo wake wa mwisho akiwa Chelsea ulikuwa wa maumivu, baada ya kuumia bega wakati wakipoteza kwenye fainali ya Kombe la FA dhidi ya Arsenal.

Alifanyiwa upasuaji na hakuweza kucheza kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Chelsea ikichezea kichapo kutoka kwa Bayern Munich, Jumamosi.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Pedro aliandika kwa kuwashukuru mashabiki wa Chelsea na mafanikio aliyoyapata pale Stamford Bridge, tangu alipojiunga nayo mwaka 2015 akitokea Barcelona.

"Baada ya miaka mitano ya kuvutia nikiwa Chelsea sasa nimefikia mwisho," aliandika.

"Naishukuru klabu na bodi, makocha na wachezaji wenzangu niliocheza nao na bila kuwasahau mashabiki: Asanteni kwa uzoefu nilioupata. Nilikuwa na furaha kubwa hapa, mlinifanya nijisikie nyumbani."

Pedro alikuwa kwenye kikosi cha Chelsea chini ya Antonio Conte kilichotwaa taji la Ligi Kuu ya England msimu wa 2016-17, huku pia akiwa ameshinda taji la Europa na klabu hiyo ya London.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# WILLIAN AAGA CHELSEA, RASMI AIBUKIA ARSENAL

## ●●● Moyo wangu unawashukuru wote na Mungu awabariki sana, asanteni sana...

**LONDON,** England

WILLIAN amethibitisha anaondoka Chelsea, huku akikaribia kukamilisha usajili wa miaka mitatu kule Arsenal.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, anaondoka pale Stamford Bridge baada ya kufikia mwisho kwa mkataba wake wa miaka saba, huku Chelsea ikiwa tayari kumpa mkataba mpya wa miaka miwili, huku yeye akitaka mitatu.**

Aliandika barua ya wazi kwa mashabiki akithibitisha kuondoka kwake baada ya Chelsea kutolewa na Bayern kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora, Jumamosi.

"Ilikuwa miaka saba ya kuvutia. Agosti mwaka 2013 wakati nilipopata ofa kutoka Chelsea, nilishawishika kwamba hapa ndio sehemu ambayo natakiwa kucheza," aliandika.

"Leo nakubali kwamba, yalikuwa maamuzi bora zaidi kwangu. Kulikuwa na nyakati nyingi za furaha, baadhi huzuni, kulikuwa na mataji na mara zote nilikuwa imara.

"Bado ukiacha mataji, nimejifunza mengi kuhusu mimi mwenyewe. Nimeimarika na kuwa mchezaji bora na mtu safi.

"Katika kila mazoezi, katika kila mchezo, kila dakika niliyotumia kwenye vyumba vya kubadilishia nguo, mara zote nilikuwa najifunza.

"Kwa uhakika nina furaha kubwa na mashabiki wa Chelsea kwa namna walivyoniunga mkono na walivyonikaribisha Stamford Bridge na sapoti yao kwa kipindi chote nikiwa klabuni hapa.

"Kulikuwa pia na shutuma, kitu ambacho ni cha kawaida, kitu muhimu ni kwamba yote hayo yalikuwa yakifanyika kwa ajili ya manufaa ya klabu.

"Muda sasa umefikia natakiwa kusonga mbele. Kwa kweli nitawamisi sana wachezaji wenzangu. Nitawamisi wote walionitendea vizuri klabuni na nitawamisi sana mashabiki.

"Moyo wangu unawashukuru wote na Mungu awabariki sana, asanteni sana."

Na kwa sasa anapewa nafasi kubwa ya kujiunga na kikosi cha Arsenal kinachonolewa na kocha, Mikel Arteta na inaaminika kwamba raia mwenzake wa Brazil, Edu ambaye ni Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, ndiye sababu kubwa kwa Willian kwenda kwa 'Washikabunduki' hao.

## ZISIKUPITE

### BARCA WAMTAKA SILVA

BARCELONA wanatumaini kumshawishi kiungo wa kati Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 25, aondoke Manchester City na wanaweza kuwapatia ofa ya mchezaji mwenzake wa kimataifa wa Ureno, Nelson Semedo mwenye miaka 26, kama sehemu ya dili hilo. ***(Telegraph)***

### ARTETA KUMUUZA TORREIRA

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anajiandaa kumuuza kiungo wa Uruguay, Lucas Torreira mwenye umri wa miaka 24, ili kupata fedha za kumsajili kiungo wa Atletico Madrid na Ghana, Thomas Partey, 27. ***(Express)***

### CITY JICHO KWA KOULIBALY

MANCHESTER City wanamatumaini wapinzani wao Manchester United kutangaza kwamba hawana mpango wa kumsajili mlinzi wa kati wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 29, ili kuepuka vita ya ofa. ***(Manchester Evening News)***

### LIVER YAMUWANIA BROOKS

MABINGWA wa Ligi Kuu ya England, Liverpool wanapanga kumsajili kiungo wa kati wa Wales, David Brooks mwenye umri wa miaka 23, kwa pauni milioni 35. ***(Sun)***

### MARTINEZ KUONDOKA ARSENAL

GOLIKIPA Emiliano Martinez mwenye umri wa miaka 27, ameitahadharisha Arsenal kwamba anaweza kuondoka katika timu hiyo kwa ajili ya kupata muda zaidi wa kucheza ili apate namba kwenye kikosi cha Argentina. ***(Continental, via Evening Standard)***

### KING LULU PSG, ROMA

MSHAMBULIAJI wa Bournemouth, Joshua King analengwa na timu ya Ufaransa Paris St-Germain, wapinzani wa Italia, Lazio na Roma wakiwa wanamtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway mwenye umri wa miaka 28. ***(Sun)***

### TSIMIKAS PIGO LEICESTER

UWEZEKANO wa Kostas Tsimikas wa kuhamia Liverpool ni pigo kwa Leicester, ambao walikuwa wamempanga kama mchezaji atakayechukua nafasi ya Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 23, mlinzi huyo ataondoka kujiunga na Chelsea. ***(Leicester Mercury)***

### LIVER, TSIMIKAS PAZURI

LIVERPOOL wamekubaliana na Olympiakos kutoa pauni milioni 11.75 kwa ajili ya usajili wa mlinzi, Kostas Tsimikas mwenye umri wa miaka 24, lakini bado hawajafikia makubaliano binafsi na mchezaji mwenyewe. ***(Liverpool Echo)***

### ARSENAL WATETA NA OZIL

ARSENAL wapo tayari kulipa pauni milioni 18 zilizosalia kwenye mkataba na kiungo wa kati Mjerumani, Mesut Ozil ambao unaisha mwakani, au kumpatia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 mshahara wa pauni 350,000- kwa wiki iwapo atahamia katika klabu nyingine. ***(Mirror)***

### GOMES KWA MKOPO BOAVISTA

KIUNGO wa zamani wa Manchester United, Angel Gomes mwenye umri wa miaka 19, amejiunga na Lille wiki iliyopita, lakini Muingereza huyo atatumia msimu ujuo kucheza kwa mkopo katika Klabu ya Boavista ya nchini Ureno. ***(Guardian)***

## Wachezaji 10 wa kigeni ruksa-Serikali

**Na Adam Fungamwango**

SERIKALI imeridhia wachezaji wa kigeni wanaocheza soka la kulipwa nchini kubakia 10 kwa kila klabu inayotaka kusajili kama ilivyokuwa awali.

Akitangaza uamuzi huo jana, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrisons Mwakyembe, amesema serikali imekubali kuendelea kuruhusu idadi 10 ya wachezaji wa kigeni baada ya kuzingatia maoni yaliyotolewa na wadau wengi.

Dk. Mwakyembe alisema kati ya watu 977 waliotoa maoni kwa njia mbalimbali, 809 wametaka idadi ya wachezaji 10 iendelee kuwapo.

Ikumbukwe kuwa wizara hiyo ilianzisha mchakato wa wadau kutoa maoni yao ya kutaka kuendelea kuwa na wachezaji 10 wa kigeni au ipunguzwe.

Hata hivyo, waziri huyo amesema kuwa idadi ya wachezaji wanaotakiwa kuanza mechi itabaki chini ya Baraza la Michezo Nchini (BMT). Pia amesema bado wizara kwa kushirikiana na BMT na wadau wa soka watakaa kujadili aina ya viwango vya wachezaji wanaopashwa kusajiliwa na kucheza nchini.

"Angalau nchi zilizopo katika nafasi 50 kwa Shirikisho la Soka Duniani (Fifa) ndiyo tusajili huko hata Daraja la Kwanza, ingawa bado si sheria ni maoni tu. Ni vema pia aina ya wachezaji watakaosajiliwa wawe na uwezo mkubwa," alisema.

Aidha, wizara imeagiza kuwa watu wanaoajiriwa nchini wawe na ulazima wa kujifunza, au kufundishwa lugha ya Kiswahili.

## ZFF yazitaka klabu kuomba leseni

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limefungua milango ya kukaribisha maombi ya leseni za klabu kwa upande wa Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja na Pemba kwa msimu wa 2020/21.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Leseni za Klabu wa ZFF, Mbarouk Othaman, alisema mchakato huo umeanza rasmi jana na utafungwa rasmi Septemba 9, mwaka huu.

Alisema klabu zote za Ligi Kuu na Kanda, zinatakiwa kuomba leseni hiyo kwa wakati pamoja na kuzingatia masharti yaliyopo katika fomu hizo ili ziweze kushiriki ligi ya msimu mpya unaotarajiwa kuanza karibuni.

Alisema kwa klabu ambazo zitakuwa zinadaiwa na wachezaji, hazitapewa leseni ya kushiriki ligi kwa msimu huu na kwamba ZFF litatilia mkazo suala hilo.

"Klabu zinatakiwa kuomba leseni kwa wakati maalum ambao ZFF wameweka ili kuepusha usumbufu pamoja na kufanya taratibu zote kwa wakati, hivyo ZFF haitaongeza muda kwa klabu za Ligi Kuu kwa kuwa wao ligi wamemaliza mapema tofauti na Daraja la Kwanza Kanda ambao wao wanaendelea na ligi," alisema.

# YONDANI, ABDUL WAZIINGIZA VITANI GWAMBINA, NAMUNGO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI klabu ya Namungo ikisema kuwa itasajili wachezaji wanane kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu na mechi za kimataifa, wachezaji wawili walioachwa na Yanga, Kelvin Yondani na Juma Abdul huenda wakajiunga na timu hiyo licha ya kuhusishwa Gwambina FC iliyopanda daraja msimu huu.

**Mwenyekiti wa klabu hiyo, Hassan Zidadu, amesema wanatarajia kusajili wachezaji nane kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho Afrika (Caf) wenye uwezo wa kuwasaidia kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa.**

"Tumeshaanza mchakato wa usajili kwa wachezaji wapya ili kuongeza nguvu kikosini, lakini tunawaongezea mikataba wachezaji wa zamani ambao muda wao wa mikataba umemalizika, lengo ni kufanya vema kwenye michuano ya Ligi Kuu na kimataifa kwa sababu ikumbukwe kuwa tunawakilisha nchi, hivyo usajili ni lazima uwe wa kimataifa kwa wachezaji wa nje na wa ndani wawe wazuri na wazoefu, kwa hiyo mashabiki wetu watulie, wasihofu kuhusu usajili," alisema mwenyekiti huyo.

Ingawa hakutaja ni wachezaji gani ambao imeanza mchakato wa kuwasajili, lakini habari za ndani zinaeleza kuwa klabu hiyo iko kwenye mazungumzo na Yondani na Abdul ambao hivi karibuni waliachwa na klabu ya Yanga baada ya kutoafikiana kwenye mchakato wa kuongeza mkataba.

Inadaiwa kuwa lengo la Namungo kutaka kusajili wachezaji hao haswa ni kutokana na kuwa na uzoefu kwenye mechi za kimataifa ambazo inakwenda kucheza, huku wachezaji wake wengi wakiwa hawana uzoefu huo.

Namungo ambayo imeanza kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza msimu huu, itaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika ambayo ratiba yake itatolewa baadaye mwaka huu.

Hata hivyo, zipo taarifa kuwa wachezaji hao pia wanawaniwa na Gwambina FC ambao nao wameonyesha nia ya kuwasajili na mazungumzo kati ya pande mbili yanaendelea.



Mfanyakazi wa Benki ya CRDB, Joyce Loth (kushoto), akimkabidhi vifaa vya kutumia katika mbio za Marathon, Ibrahim Kingamila, baada ya kujiandikisha kushiriki mbio hizo za kuhamasisha uchangiaji wa fedha kwa ajili ya watoto wenye magonjwa ya moyo zitakazofanyika Jumapili wiki hii jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kiatu Ligi Wanawake kutua JKT Queens

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya Simba Queens kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake, imeshindwa kufikia rekodi kama ya timu yao ya wanaume, Simba iliyobeba 'ndoo' ya Ligi Kuu sambamba na straika wao, Meddie Kagere kubeba Kiatu cha Dhahabu kwa kuibuka mfungaji bora wa ligi hiyo.

Hadi sasa mshambuliaji wa JKT Queens, Fatma Mustaf yupo kileleni mwa orodha ya wafungaji bora katika ligi hiyo msimu huu akiwa na mabao 30 akifuatiwa na wachezaji wenza wa timu hiyo, Asha Rashid mwenye mabao 19 sambamba na Stumai Abdallah aliyetupia mara 18.

Washambuliaji wa Simba Queens, Mwanahamis Omar na Oppah Clement wapo mbali katika orodha hiyo wakiwa na mabao 17 sambamba na Amina Ramadhani (Ruvuma Queens) na Aisha Khamis (Alliance Girls).

Hivyo, wakati huu ligi hiyo ikiwa imetarajiwa kumalizika kesho, ni wazi Fatma wa JKT Queens ana nafasi kubwa ya kutwaa kiatu hicho msimu huu.

Hata hivyo, licha ya Simba Queens kushindwa kufikia rekodi hiyo ya kaka zao ya kutwaa ubingwa na straika wao kubeba Kiatu cha Dhahabu, kinadada hao wapo katika nafasi nzuri ya kuwazidi kwa rekodi ya kupoteza michezo miwili tu endapo haitapoteza mechi yao ya mwisho kesho.

Hadi Simba inamaliza ligi imepoteza mechi nne, huku ikifumania nyavu mara 85 na kuruhusu nyavu zao kutikiswa mara 33 kwenye ligi hiyo iliyoshirikisha timu 20.

Lakini kwa Simba Queens ambayo imebakiza mechi moja dhidi ya TSC Queens ya jijini Mwanza, hadi sasa imepoteza mchezo mmoja tu huku ikifumania nyavu mara 72 na kuruhusu mabao 12 katika ligi hiyo iliyoshirikisha timu 12.

# Michezo

Jumanne Agosti 11, 2020

Nipashe




Willian aaga Chelsea, aibukia Arsenal

UKURASA 22

IMEISHA HIYO...






Picha mbili tofauti zikimwonyesha Bernard Morrison wakati akisaini mkataba Simba na akionyesha mkataba wake na Yanga akiwa na Mkurugenzi wa Uwekezaji GSM Mhandisi Hersi Said, ambaye anayeidhamini klabu hiyo kupitia kampuni hiyo. Sakata hilo lilitarajiwa kumalizika jana. **PICHA: MAKTABA**

## Morrison azianika Simba, Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa klabu kongwe nchini Simba na Yanga, wamepata wakati mgumu jana wa kulisogelea lango la Ofisi za Shirikisho la Soka nchini wakati Kamati ya Hadhi ya Wachezaji ya Shirikisho la Soka nchini (TFF) ikisikiliza kesi ya kiungo mshambuliaji wa Yanga, Bernard Morrison ambaye yupo kwenye mvutano na timu yake kuhusu suala la usajili.

Yanga inadai kuwa na mkataba wa miaka miwili na Morrison, wakati yeye akida saini yake ilighushiwa huku akiwa tayari ametia saini kuitumikia Simba msimu ujao.

Sakata hilo limevuta hisia za mashabiki wengi wa soka kila mmoja jana akiwa na kiu ya kutaka kujua nani ataibuka kidedea wakati huu Simba ikiwa tayari imeshamtambulisha.

Tangu asubuhi wadau wengi wa soka walijitokeza ili kujua kinachoendelea na kuweka kambi nje ya makao hayo yaliyopo Karume, Ilala jijini Dar es Salaam, lakini walikutana na ulinzi mkali kutoka Jeshi la Polisi na kuzuiwa kuingia ndani kwa wale wote ambao hawakuwa na ahadi na TFF.

Hali hiyo haikuwa kwa wadau wa soka ama mashabiki tu, bali hata waandishi wa habari hawakuruhusiwa kabisa kuingia katika lango kuu la TFF na kikao hicho kiliendelea huku hali ikiendelea kwa mtu kupenya ndani ama kujua kinachoendelea. Hadi Nipashe linakwenda mitamboni bado haikujulikana mbivu mbichi kuhusu sakata hilo.

# Yanga yaitiwa Chama, Fraga

**Na Saada Akida**

### ●●● Uongozi Simba watangaza dau, wachezaji hao kila mmoja akikiri bado ana mkataba wa...

WAKATI viungo wa Simba, Mzambia Claotus Chama na Mbrazil Gerson Fraga wakizidi kuhusishwa na kujiunga na wapinzani wao, Yanga, 'Wekundu wa Msimbazi' hao, wametoa kauli 'pendwa' kwa watani zao kwa kuwaita mezani kuteta ili kumalizana, imeelezwa.

**Tangu kuibuka kwa sakata la kiungo wa Yanga, Mghana Bernard Morrison kutangazwa kutia saini mkataba wa kujiunga na Simba, klabu hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani nayo imekuwa ikihusishwa na kutaka kuwasajili Chama na Fraga.**

Taarifa hizo zilikolezwa zaidi juzi baada ya Yanga kufanikiwa kuipata huduma ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mbatha Mazingiza, zikidai kituo kinachofuata kwa Chama ni Jangwani kuungana na bosi huyo.

Hata hivyo, Crescentius Magori, ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba na Mshauri wa Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, Mohammed "Mo" Dewji, amesema watani zao hao wanaweza kuwasajili wachezaji hao kwa sasa kama tu watakubaliana dau wanalolitaka.

Magori aliliambia Nipashe jana kuwa wachezaji hao bado wana mikataba na Simba na kwamba Chama ambaye amekuwa akihusishwa zaidi na Yanga, ana uhakika huo kwa kuwa mchezaji huyo alitia saini mkataba wake mbele yake kipindi yeye akiwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo (CEO).

"Kama wanamtaka waje mezani, hatukatai kumuuza, endapo wana Dola 800,000 walete tutawauzia, kwani bado tuna mkataba wa mwaka mmoja naye," Magori alisema.

Nakuongeza kuwa wakati huu Chama akiwa kwao Zambia kwa mapumziko mafupi, amemueleza kuna watu wamekuwa wakimfuata wakala wake kutaka huduma yake.

Naye Ofisa Habari wa Simba, Hajji Manara alitoa ufafanuzi zaidi akisema mwaka jana, nyota huyo na wengine akiwamo Meddie Kagere waliongeza mkataba wa mwaka mmoja utakaomalizika Julai 2021.

"Mkataba wa awali wa Chama ulikuwa unaisha Julai 2020, mwaka jana aliongeza mwaka mmoja ambao sasa utamalizika 2021, pamoja na nyota wetu wengine wanaotajwa.

"Yanga au timu yoyote kama wanamtaka Chama na wachezaji waliokuwa na mikataba walete barua ya kuomba kumsajili, sisi hatuweza kwenda kwa Feisal Toto mwenye mkataba na kumsajili," alisema Manara.

Kwa upande wa Fraga, akizungumza na Nipashe kwa simu jana kutoka kwao Brazil alipo kwa mapumziko mafupi, alikanusha taarifa zilizozagaa kuwa ameuandikia barua uongozi wa Klabu ya Simba kuomba kuondoa kama ambavyo inadaiwa kupitia mitandao ya kijamii na vyombo mbalimbali vya habari (si Nipashe).

Alisema bado yupo Simba na hajamaliza mkataba, na sasa yupo kwao kwa mapumziko mafupi na atarejea mapema kabla ya muda wa kuingia kambini.

"Hizo taarifa za kuandika barua si kweli, mimi ni mchezaji halali wa Simba, mkataba wangu umebaki miezi sita, nitarudi kuitumikia timu yangu kwa msimu ujao," alisema kiungo huyo.

Simba inatarajia kuingia kambini Jumatatu ijayo kwa ajili ya maandalizi ya mechi yao ya Ngao ya Jamii dhidi Namungo itakayopigwa Agosti 29 katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, na kisha timu hiyo kuunganisha kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu inayotarajiwa kuanza Septemba 6, mwaka huu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >